# Mwongozo kwa Waalimu

## Wakati na Biblia Daraja la tatu na la nne

Mfululizo wa C
Somo la kwanza hadi la sita

www.besweb.com

## Bible Educational Services

Registered Charity UK (No 1186004)
Imesajiliwa kama shirika la Hisani Uingereza (Namba 1186004)

**Dhamira**
Kuandaa masomo ya Biblia kwa ajili ya wadau ili kutumika kuwakilisha kweli ya Yesu Kristo kwa kizazi kijacho ulimwenguni kote.

**Maono**
Kufikia kizazi kijacho kwa lugha zao kwa kutumia mtaala wetu kamili kwa kukuza na kusaidia mtandao wa kimataifa wa wabia wanaojitolea.

## HABARI KWA UJUMLA

**Bible Educational Services hufanya nini:**

Bible Educational Services (BES) huchapisha masomo ya Biblia ya “Wakati na Biblia/Bibletime”, “Maisha Mapya/New Life” na “Wakusanyaji/Gleaners” kwa Lugha ya Kiingereza na kusaidia vituo vya Shule ya Biblia kwa njia ya Posta pamoja na mashirika mengine ya namna hiyo yanayotumia masomo ya BES huko Uingereza na nchi zingine. BES hufanya hivi kwa kutembelea, kutoa ushauri, kutoa mafunzo na kuunganisha mashirika haya na mengine. Sasa hivi, BES inafanya kazi na vikundi mbalimbali kutoka nchi zingine, vinavyohusika na kutafsiri, kubuni, kuchapisha na kusambaza masomo. Masomo haya yanatolewa bure kabisa kwa kila mtoto.

Kwa mara ya kwanza, masomo ya Wakati na Biblia yalitumika huko Kusini mwa Ireland (Uingereza) miaka sitini iliyopita. Bible Educational Services (BES) wamechukua jukumu la uhariri wa masomo ya Wakati na Biblia kwa lugha ya Kiingereza na Lugha zingine. Kwa muda mrefu, Masomo ya Wakati na Biblia (Bibletime) yalichapishwa kwenye muundo wa A4 ambao uliwawezesha wanafunzi kutoka baadhi ya maeneo kutuma masomo yao kwenye kituo cha BES kwa ajili ya kusahihishwa kila baada ya wiki nne. Hivi karibuni, masomo ya miezi sita yamechapishwa kwa muundo wa A5. Muundo huu umefanya utumiaji wa masomo haya uwe rahisi na wakufaa zaidi kwa makanisa na shule ambazo hazina ufanisi mzuri wa mfumo wa njia ya posta. Tunawashukuru Every Home Crusade au Revival Movement huko Belfast Uingereza kwa kutuwezesha kufanya hivi.

Masomo ya BES ni ya kipekee kwa sababu yameandaliwa na vikundi mbalimbali kutoka makanisa na shule mbalimbali ambavyo vimezingatia mtaala (Syllabus). Masomo yamepangiliwa vizuri na yanamruhusu mwanafunzi kuyatumia kwa muda mrefu hadi atakapotimiza umri wa miaka ishirini. Masomo yanapatikana katika madaraja matano ambayo yamezingatia umri tofauti. Nayo ni, masomo kwa ajili ya watoto wa chekechea (chini ya miaka mitano), miaka mitano hadi saba, miaka nane hadi kumi, miaka kumi na moja hadi kumi na mitatu na miaka kumi na minne hadi kumi na sita. Kuna Mtaala wa miaka mitatu katika kila kikundi cha umri (angalia ukurasa wa 6). Vikundi hivi vya umri vinaweza kutofautiana kulingana na uwezo tofauti wa watoto. Rasilimali na masomo ya Wakati na Biblia yanawapa watoto fursa ya kujifunza Neno la Mungu, kujifunza Habari za Biblia na kujifunza kukabiliana na changamoto zinazotokea maishani mwao kulingana na mwongonzo wa Injili ya Bwana Yesu Kristo.

Nakala zilizochapishwa za masomo kwa Lugha ya Kiingereza zinapatikana kwenye tovuti ya BES /BES website – www.besweb.com au kwa katibu ofisi ya BES Uingereza. Yanapatikana pia kwa lugha zingine kwenye tovuti. Kwenye tovuti kuna nyaraka muhimu kwa mtu yeyote au shirika linalopenda kushirikiana nasi.

## Anuani za mawasiliano za BES

**Ofisi ya Uingereza (Northern Ireland) (Mhifadhi wa masomo yote ya Kiingereza)**
37a Belmore Street, Enniskillen, Northern Ireland BT74 6AA
Simu: +44 286 632 2462

**Katibu wa Uingereza**
Bw. Stephen Gillham,
Barua pepe: stephen.gillham@besweb.com

Tovuti: www.besweb.com
Barua pepe: info@besweb.com

**Mshirika Tanzania (Tanzania Partner)**
World Vision Tanzania
S.L.P. 6070 Arusha, Tanzania
Barua Pepe ya Mawasiliano: david_ombeni@wvi.org
Simu: +255 687 231 757

## MWONGOZO kwa WAALIMU

Mwanzoni, masomo ya Wakati na Biblia yaliandaliwa ili yatumike kwa njia ya posta kukiwepo na kituo cha Shule ya Biblia kwa njia ya posta. Sasa hivi, masomo yanaendelea kutumika kwa wingi hata kwenye sehemu ambazo hazina ufanisi wa kutumia mfumo wa posta au hakuna kabisa mfumo wa posta hasa katika makanisa na shule zilizopo Afrika, India na maeneo mengine. Mwongozo wa kufundisha umeandaliwa kwa wale wanaotumia masomo ya Wakati na Biblia katika hali kama hizo. Mwongozo wa kufundisha katika kitabu hiki umeandaliwa kutumika kwa masomo ya daraja la tatu na la nne kwa watoto wenye umri wa wastani wa miaka 11-16 na zaidi.

Kila Mwongozo wa kufundisha hufuata vifungu vile vile vya Biblia vilivyopo katika somo la Wakati na Biblia. Masomo ya Wakati na Biblia na Mwongozo vimeandaliwa vitumike kwa kila wiki. Masomo ya mwezi Aprili yanahusu Pasaka na masomo ya mwezi Desemba yanahusu Krismasi.

Baadhi ya sehemu watakuwa wanatumia masomo yaliyo katika toleo la A4 la kila wiki na wengine watakuwa wanatumia kitabu cha A5 chenye masomo 24 ndani yake. Kwa kawaida, mwalimu au kiongozi hutoa somo la mwezi toleo la A4 na kila wiki sehemu ya kazi hujazwa kanisani au shuleni au hupelekwa nyumbani na kurejeshwa wiki inayofuatia. Mwishoni mwa mwezi, mwalimu au kiongozi hukusanya somo na kwenda kusahihisha kama inavyotakiwa na kumrudishia mwanafunzi/mtoto kazi iliyosahihishwa mapema iwezekanavyo.

Unapotumia kitabu, mwisho wa kila kipindi, vitabu hukusanywa na kusahihishwa. Tumegundua katika sehemu nyingi kuwa, hili haliwezekani. Hivyo basi, pale darasani masomo yanaweza kugawanywa kwa wanafunzi wengine na mwalimu au kiongozi ataongoza usahihishaji wa somo na wanafunzi watasahihisha masomo ya rafiki zao na kutoa maksi. Nyuma ya kitabu kuna sehemu kwa ajili ya kuweka maksi ya kila somo la mwezi na pia mahali pa maoni kuhusu maendeleo ya mwanafunzi. Pia kuna cheti ambacho mwanafunzi anaweza kupewa kinachoonesha asilimia ya alama ambazo mwanafunzi amepata kwa masomo ya miezi sita.

Tutashukuru kama tutapata mrejesho kuhusu matumizi ya Miongozo ya Waalimu na kwa ajili ya vitabu vya Wakati na Biblia na mrejesho huo utumwe kwa stephen.gillham@besweb.com.

## MAANDALIZI KWA WAALIMU

Hatupendi kutoa shinikizo na kutokuwapa waalimu fursa ya kufanya mambo kwa njia zao wenyewe kulingana na mawazo na mipango yao wenyewe. Haya ni mapendekezo yanayoweza kutumika kwenye utumiaji wa masomo ya Wakati na Biblia.

- **Elewa habari vizuri –** Waalimu wanapaswa kuelewa habari ya Biblia vizuri kwa kadri iwezekanavyo na vile vile somo la Wakati na Biblia linaloendana na habari hiyo ya Biblia. Ni jambo zuri kwa mwalimu kuKamilisha Somo la Wakati na Biblia kabla ya kipindi. Mwongozo wa kila somo unapaswa kutumiwa kwa umakini kama chombo cha kumsaidia mwalimu anapojiandaa kwa ajili ya somo.
- **Elewa funzo ambalo watoto wanastahili kupata au kujifunza –** Juu ya kila mpangilio wa somo utaona maneno ‘Tunajifunza kuwa’ ikifuatiwa na makusudio mawili ya kujifunza ambayo tunatumaini kwamba watoto watayaelewa baada ya kumsikiliza mwalimu akifundisha na kuKamilisha Somo la Wakati na Biblia. Kusudio la kwanza la kujifunza linahusu ufahamu wa habari na la pili linamtia moyo mtoto kufikiri juu ya ufahamu huo, kuutumia na kuuitikia. Makusudio haya ya kujifunza ni sentensi kamilifu na fupi ya mawazo au kweli kuu zinazofundishwa katika somo. Waalimu wanaweza kuzitumia kwa ajili ya tathimini zao binafsi za ufundishaji na mafunzo ambayo watoto wamepata.
- **Toa Utangulizi –** Kwa masomo yote, tunaanzia mahali ambapo watoto wapo katika uzoefu wao wa hali husika. Tumependekeza njia kadhaa ambazo zinaweza kutumika kufanya utangulizi wa habari ili kuwawezesha watoto kuhusika katika kujadili mwanzo wa habari.
- **Fundisha –** Tumetoa dondoo muhimu katika habari. Tunaamini kwamba waalimu hawatazinukuu wakati wanafundisha habari lakini watakuwa na uelewa mzuri wa habari na wataweza kuifundisha katika njia inayofurahisha na kusisimua. Mwalimu atahitaji watoto waelewe mafunzo muhimu kutoka kwenye habari na kuwasaidia kuuelewa mwitikio watakaoupata kutoka kwenye habari waliyojifunza. Kwa usahihi, tumejaribu kuweka pamoja baadhi ya maelezo kwa ajili ya kufundisha habari. Haya yameandikwa katika maandishi *YA MCHALAZO (Italics)*.
- **Jifunze –** Kuna Mstari muhimu ambao umewekwa katika kila habari. Katika baadhi ya maeneo, kuna Mistari muhimu miwili. Mstari huu ulioongezwa unaweza kuwa rahisi kwa watoto kujifunza. Tunatumaini kwamba, watoto watajifunza Mistari muhimu na watakumbushiwa mstari huo mara nyingi iwezekanavyo ili waanze kujenga ufahamu wa Mistari muhimu ya Biblia.

- **Kamilisha –** Katika mazingira ya shule, utatambua uwezo wa watoto kwenye kukamilisha kazi na kiasi cha usaidizi ambao wanauhitaji kutoka kwa mwalimu. Kwa baadhi yao, itahitajika mwalimu asome maandishi katika somo na watoto kufuatilia habari ambayo sasa watakuwa wanaielewa. Watoto wengine wanaweza kusoma maandishi ya somo peke yao. Kwa hali yoyote kati ya zilizotajwa, ni wazo zuri kuwahamasisha watoto wawe makini na kuwapa maelekezo muhimu yanayohusiana na maswali. Kama unatumia masomo ya Wakati na Biblia katika maeneo ambayo siyo shule, ni muhimu uwepo ili watoto wasichukulie masomo kama kazi isiyo na mvuto au kama mtihani. Masomo haya yanapaswa kuwa ya kufurahisha na kutia moyo. Ni muhimu kuwasifia watoto wanapoendelea kufanya masomo na kujibu maswali.
- **Kumbuka –** Tunashauri matumizi ya maswali mafupi na maigizo ili kuwasaidia watoto kujifunza na kurudia habari ili kuielewa vyema.
- **Kuonesha –** Tunatambua kuwa katika baadhi ya mazingira, sio rahisi kupata vielelezo au video. Lakini, ni muhimu kadri iwezekanavyo kuwa na picha au vitu vinavyoweza kuwasaidia watoto kuielewa habari vizuri zaidi. Vielelezo vitakuwa muhimu sana wakati ambapo mwalimu anaelezea habari. Kadri iwezekanavyo kwenye kila somo, tumetoa maelezo kuhusu picha kutoka kwa picha za www.freebibleimages.org (FBI) ambazo zinaweza kupakuliwa bure kwenye tovuti yao. Mwishoni mwa Mwongozo huu kuna viambatanisho vyenye viungo (hyperlinks) vya picha kadhaa kutoka kwenye tovuti ya Free Bible Images ambazo zinafaa kila habari ya Biblia.

  Kama kuna kinakilishi (photocopier), baadhi ya picha za Bibletime zinaweza kufanywa kuwa kubwa, kupakwa rangi na kutumiwa kufundisha.

## Kupangilia Muda

- **Ratiba –** Tumeweka ratiba sawa kwenye mwongozo wa kufundisha kila somo lakini mwalimu anaruhusiwa kubadilisha ratiba hii mara kwa mara kulingana na mahitaji ya darasa lake/ watoto anaowafundisha.
  1. Utangulizi na kuwaambia watoto habari husika – Takriban dakika 15
  2. Kufundisha Mstari muhimu – dakika 5 hadi 10
  3. Kujaza nakala ya somo – dakika 20
  4. Maswali na shughuli zinginezo- dakika 5 hadi 10

Kumbuka msemo muhimu:

“Niambie na nitasahau,
Nioneshe na nitakumbuka,
Nihusishe na nitaelewa”

## Mtaala wa Wakati na Biblia

| | Daraja 0 (Chekechea/ Kabla ya Kuanza Shule) Daraja la Kwanza (Miaka mitano hadi saba) Daraja la Pili (Miaka nane hadi kumi) | Daraja la Tatu (Miaka kumi na mmoja hadi kumi na mitatu) | Daraja la Nne (Miaka kumi na minne na zaidi) |
|---|---|---|---|
| SOMO LA KUANZIA | Somo la kuanzia – Utangulizi | Somo la kuanzia – Utangulizi | Somo la kuanzia – Utangulizi |
| MFULULIZO WA A | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Ibrahimu<br>6. Ibrahimu<br>7. Petro<br>8. Petro<br>9. Yakobo<br>10. Wakristo wa Kwanza<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo<br>2. Nuhu<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maombi<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mwanzo na Kuanguka<br>2. Matukio ya Kwanza-Mwanzo<br>3. Petro<br>4. Petro- Msalaba<br>5. Petro<br>6. Ibrahimu<br>7. Yakobo<br>8. Maisha ya Ukristo<br>9. Paulo<br>10. Paulo<br>11. Paulo<br>12. Habari ya Krismasi |
| MFULULIZO WA B | 1. Maisha ya kwanza ya Kristo<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Mifano<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yusufu<br>7. Yusufu<br>8. Walioandika vitabu vya Injili<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Musa<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Mifano<br>2. Miujiza<br>3. Bethania<br>4. Msalaba<br>5. Wakristo wa kwanza<br>6. Yakobo na familia yake<br>7. Yusufu<br>8. Matendo ya Mitume 2: 42 – Njia iliyoko mbele<br>9. Musa<br>10. Musa<br>11. Amri<br>12. Habari ya Krismasi |
| MFULULIZO WA C | 1. Danieli<br>2. Miujiza zaidi<br>3. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu na Samweli<br>6. Daudi<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Yona<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Watu ambao Yesu alikutana nao<br>3. Miujiza zaidi<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8 Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu ambao Mungu aliwatumia – Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi | 1. Danieli<br>2. Maneno ya Kristo<br>3. Nguvu za Bwana<br>4. Kifo cha Kristo<br>5. Ruthu<br>6. Samweli<br>7. Daudi<br>8. Yoshua<br>9. Elia<br>10. Elisha<br>11. Watu zaidi wa Agano la Kale<br>12. Habari ya Krismasi |

| | C1 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Kwanza – Danieli<br>Mada – Nchi ya ugenini | C1 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Kwanza – Danieli<br>Mada – Kumtumikia Mungu |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Danieli 1: 1-21***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 6: 33***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu bado anatawala hata nyakati ngumu zinapokuja.<br>2. Daniel alisimamia kile alichokiamini. | **Neno la Biblia:** ***Danieli 1: 1-7, 2: 1-49***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Danieli 2: 28***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Danieli na marafiki zake walimtumaini Mungu atawasaidia na kuwapa majibu waliyohitaji.<br>2. Mungu bado anatawala, hata nyakati ngumu zinapokuja. |
| TOA UTANGULIZI | Tafuta picha mbili za vyakula, moja ikionyesha matunda yenye afya na mboga za majani na nyingine karamu ya vyakula vya kifahari. Waulize watoto wangependelea kula nini na kwa nini. | Waambie wanafunzi wafikirie namba kati ya 1 na 20 na wafanye wanafunzi wengine kukisia ni namba gani wamechagua. Elezea kwamba hatuwezi kujua watu wengine wanafikiria nini. Katika somo hili, Mfalme Nebukadneza alikuwa akitarajia wachawi wake wajue ndoto yake bila yeye kuwaambia. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Mfalme Nebukadneza alivamia Yerusalemu na kuchukua vitu vya hekalu na mateka na kurudi Babeli.***(1: 1-2)***<br>2. Ashpenazi, ofisa mkuu wa makao ya mfalme, alichagua vijana werevu, wenye sura nzuri, na wenye hekima ili kuwafundisha utumishi kwa ajili ya mfalme kwa miaka mitatu.***(1: 3-5)***<br>3. Danieli hakutaka kula chakula cha kifahari cha mfalme kwa sababu kilikuwa kimetolewa sadaka kwa sanamu. ***(1: 8)***<br>4. Daniel alikubali kula mtama na maji badala yake, kwa kipindi cha majaribio cha siku kumi. ***(1: 11-14)***<br>5. Mwishoni mwa kipindi cha majaribio Danieli na marafiki zake walionekana kuwa katika hali nzuri zaidi ya kimwili kuliko wale waliokula chakula cha kifalme. ***(1: 15-16)***<br>6. Mungu aliwapa Danieli na rafiki zake maarifa na ufahamu wa kila aina ya fasihi na elimu. Danieli alipewa hata uwezo wa kueleza maana ya maono na ndoto. ***(1: 17)***<br>7. Juhudi ya kazi ya Danieli na rafiki zake ilifanikiwa, na mfalme akavutiwa. Akawaona kuwa bora mara kumi kuliko waganga wote katika ufalme wake wote.***(1: 20)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Nchi ya ugenini. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Mfalme Nebukadneza alivamia Yerusalemu na kuchukua vitu vya hekalu na mateka na kurudi Babeli.***(1: 1-2)***<br>2. Ashpenazi, ofisa mkuu wa makao ya mfalme, alichagua vijana werevu, wenye sura nzuri, na wenye hekima ili kuwafundisha utumishi kwa ajili ya mfalme ***(1: 3-5)***<br>3. Mfalme alifadhaishwa sana na ndoto. Aliwataka wenye hekima wamweleze ndoto yake na maana ya ndoto hiyo. ***(2: 1-2)***<br>4. Mfalme alisema kwamba ikiwa mamajusi hawangemkumbusha ndoto hiyo na kumweleza, basi wote wangekufa. Kwa hiyo, maisha ya Danieli na rafiki zake pia yalikuwa hatarini. ***(2: 13)***<br>5. Danieli alipotambua jambo lililokuwa likitokea, yeye na marafiki zake walimuomba Mungu ili awasaidie. ***(2: 18)***<br>6. Mungu alimfunulia Danieli ndoto na maana yake, naye Danieli akamsifu Mungu kwa kumpa maana ya ndoto hiyo. ***(2: 19-23)***<br>7. Danieli alipokutana na mfalme, alimwambia kwamba ni Mungu pekee awezaye kueleza ndoto hiyo. Kisha akamwambia mfalme maana ya ndoto hiyo. ***(2: 27-45)*** Ndipo mfalme akawapa Danieli na rafiki zake vyeo vya mamlaka. ***(2: 48-49)***<br>*(Pengine si busara kujaribu na kujadili maudhui halisi ya ndoto na maelezo yake)*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kumtumikia Mungu. |
| REJELEA SOMO | Ni ushauri gani unaweza kumpa Mkristo anayeanza shule mpya au anayehamia darasa tofauti? Hali yao inafananaje na Danieli na marafiki zake huko Babeli? | Danieli na rafiki zake walichukuliaje tatizo lao la kutafuta kujua kuhusu ndoto hiyo?<br>Tunapaswa kukabiliana vipi na hali ngumu?<br>***Soma Wafilipi 4: 6-7.*** |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Tunapokuwa kwenye hali mpya, je, tunasimamia lile lililo sahihi?<br>2. Je, tumejiandaa kumfuata Mungu na njia zake badala ya kuwafuata wengine wanaoweza kutupeleka mbali na Mungu?<br>3. Tunaweza kujifunza nini kutokana na habari kuhusu umuhimu wa kula chakula bora? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>Wakati mwingine tunakabiliana na hali ambayo inaonekana kuwa haiwezekani. Mungu aliweza kumsaidia Danieli na marafiki zake. Je, Mungu anaweza kutufanyia vivyo hivyo? Soma ***Luka 1: 37.*** |

| | **C1 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Pili – Danieli**<br>**Mada – Tanuru ya moto** | **C1 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Pili – Danieli**<br>**Mada – Kusimama imara katika Mungu** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Danieli 2: 48-49; 3: 1-30***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Danieli 3: 17***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Kama sisi ni Wakristo, tunapaswa kuwa tayari kusimama kwa ajili ya Mungu kwa gharama yoyote kama walivyofanya marafiki watatu wa Danieli.<br>2. Tukimtanguliza Bwana Yesu maishani mwetu, atatutunza katika maisha haya na kutupa thawabu katika siku zijazo kwa kuwa waaminifu Kwake. | **Neno la Biblia:** ***Danieli 3: 1-30***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Danieli 3: 17***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Kama vile Shadraka, Meshaki, na Abednego walivyomwamini Mungu awakomboe, tunapaswa kumtumikia Mungu kwa uaminifu.<br>2. Ni muhimu kutetea lililo sawa. |
| **TOA UTANGULIZI** | Wakumbushe watoto kwamba katika nchi ya Babeli, watu waliabudu sanamu. Sanamu katika somo hili ilikuwa sanamu iliyotengenezwa kwa dhahabu. Urefu wake ulikuwa futi 90, na upana wake ulikuwa futi 9. Nebukadneza aliamuru kwamba watu wakisikia muziki wanapaswa kuanguka chini na kuiabudu. Hata hivyo, wale vijana watatu Wayahudi, Shadraka, Meshaki, na Abednego walikataa kuabudu sanamu hiyo kwasababu walikuwa wa Mungu wa pekee na wa kweli. | Wakumbushe wanafunzi kwamba katika nchi ya Babeli, watu waliabudu sanamu. Sanamu katika somo hili ilikuwa sanamu iliyotengenezwa kwa dhahabu. Urefu wake ulikuwa futi 90, na upana wake ulikuwa futi 9. Nebukadneza aliamuru kwamba watu wakisikia muziki wanapaswa kuanguka chini na kuiabudu. Hata hivyo, wale vijana watatu wa Kiyahudi, Shadraka, Meshaki na Abednego walikataa kuabudu sanamu hiyo kwasababu walikuwa wa Mungu wa pekee na wa kweli. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Shadraka, Meshaki, na Abednego walikataa kuabudu sanamu. ***(3: 12)***<br>2. Nebukadneza aliwakasirikia na kutishia kuwatupa katika tanuru inayowaka moto. ***(3: 15)***<br>3. Shadraka, Meshaki na Abednego walimwambia Nebukadneza kwamba ikiwa wangewetupwa ndani ya tanuru, Mungu angewaokoa.***(3: 17)***<br>4. Kisha Nebukadneza akaamuru tanuru ya moto iwekwe moto mara saba kuliko kawaida na wale vijana watatu ambao ni Wayahudi watupwe humo. Tanuru ilikuwa ya moto sana kiasi kwamba watu waliowatupa wao wenyewe walikufa. Hata hivyo, mfalme alipotazama ndani, alishangaa kuona watu wanne – mmoja wao akiwa Mwana wa Mungu. ***(3: 19-25)***<br>5. Wayahudi hawakudhurika! Mfalme alivutiwa sana kiasi kwamba hakuruhusu mtu yeyote amseme vibaya Mungu wa Wayahudi. Pia aliwapandisha vyeo vijana hawa ingawa walikuwa wamekataa kumtii! ***(3: 28-30)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Tanuru ya moto. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Shadraka, Meshaki, na Abednego walikataa kuabudu sanamu. ***(3: 12)***<br>2. Nebukadneza aliwakasirikia na kutishia kuwatupa katika tanuru inayowaka moto. ***(3: 15)***<br>3. Shadraka, Meshaki na Abednego walimwambia Nebukadneza kwamba ikiwa wangetupwa ndani ya tanuru, Mungu angewaokoa. ***(3: 17)***<br>4. Kisha Nebukadneza akaamuru tanuru ya moto iwekwe moto mara saba kuliko kawaida na wale vijana watatu ambao ni Wayahudi watupwe humo. Tanuru lilikuwa la moto sana kiasi kwamba watu waliowatupa wao wenyewe walikufa. Hata hivyo, mfalme alipotazama ndani, alishangaa kuona watu wanne – mmoja wao akiwa Mwana wa Mungu. ***(3: 19-25)***<br>5. Wayahudi hawakudhurika! Mfalme alivutiwa sana kiasi kwamba hakuruhusu mtu yeyote amseme vibaya Mungu wa Wayahudi. Pia aliwapandisha vyeo vijana hawa ingawa walikuwa wamekataa kumtii!<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kusimama imara katika Mungu. |
| **REJELEA SOMO** | Jadili na watoto jinsi Mstari Muhimu unavyofupisha matukio katika somo hili.<br><br>Pia tazama Yohana 10:28 na ujadili ahadi kuu ambayo Bwana Yesu alitoa kwa wale wanaomfuata. | 1. ***Kutoka 20: 1-6*** - Soma na ujadili inachosema kuhusu kutoabudu sanamu. Shadraka, Meshaki na Abednego walitii jambo hilo. Zungumzia umuhimu wa kujua yale ambayo Biblia inafundisha kuhusu kumpendeza Mungu.<br>2. ***Matendo 5: 27-32*** - Soma na ujadili jinsi Petro na Mitume, kama vijana hawa watatu, walivyomwambia Kuhani Mkuu na Baraza kwamba watamtii Mungu na si wanadamu. ***(mstari wa 29)*** |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Ikiwa sisi ni Wakristo, tunajifunza kutokana na somo hili kwamba Bwana Yesu anaweza kutusaidia katika shida zetu au yuko pamoja nasi katika shida.<br>2. Kama vile mfalme alivyovutiwa na jinsi vijana hao walivyokuwa waaminifu kwa Mungu, vivyo hivyo wale ambao si Wakristo wanapaswa kuvutiwa na maisha na imani ya Wakristo.<br>3. Shadraka Meshaki na Abednego walikuwa tayari kuwa waaminifu kwa Mungu bila kujali gharama watakayopata. Kama Wakristo tunapaswa kuwa tayari kuishi hivi hata leo. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Imani ya vijana hawa watatu ilikuwa ya pekee. Imeitwa imani ya “hata isipokuwa hivyo”. Wakasema, ‘Mungu wetu anaweza kutuokoa, ***lakini hata isipokuwa hivyo***, bado tutakataa kusujudu. Muombe Mungu akupe imani ya namna hiyo. ***(Waebrania 11: 1)***<br>2. Shadraka, Meshaki na Abednego walikuwa marafiki na walisimama pamoja katika jaribu hili. Hakikisha unasimama pamoja na wale wanaompenda Bwana Yesu. |

| | C1 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Tatu – Danieli<br>Mada – Mkono wa ajabu | C1 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Tatu – Danieli<br>Mada – Kusema kwa ajili ya Mungu |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Danieli 5: 1-31***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Danieli 5: 23***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mfalme Belshaza, kama alivyokuwa baba yake Nebukadneza, alimpuuza Mungu katika mwenendo wake.<br>2. Ni rahisi kusahau masomo ambayo wazazi wetu wanatufundisha na masomo tunayoweza kujifunza katika Biblia. | **Neno la Biblia:** ***Danieli 5: 1-31***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Danieli 5: 23***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mfalme Belshaza alikuwa na kiburi na alikuwa amempuuza Mungu kama baba yake Nebukadneza.<br>2. Mungu ndiye anayetawala kila kitu na tunahitajika kumwamini na kumtii. |
| TOA UTANGULIZI | Fikiria baadhi ya sheria tulizo nazo katika nchi yetu, au katika shule yako. Jaribu kufikiria na uandike ujumbe wa kuvutia kwa maneno yasiyozidi MANNE. Jadili zinaweza kuwa na athari gani k.m. Huruhusiwi kukimbia Shuleni! | Fikiria baadhi ya kanuni na sheria katika nchi yako na ujadili matokeo yake ikiwa sheria hizo zitapuuzwa na kwa nini uvunjaji wa sheria lazima uadhibiwe. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Mfalme Belshaza akawafanyia karamu kubwa wakuu wake 1000. Alipuuza masomo yote ambayo baba yake alikuwa amejifunza kuhusu kumfuata Mungu. Alidai kutumia vyombo vya fedha na dhahabu kutoka katika Hekalu la Mungu huko Yerusalemu. ***(5: 1-2)***<br>2. Vidole vya binadamu vilitokea ghafla na kuandika ujumbe ukutani. Mfalme aliogopa sana. Hakuna aliyeweza kusema ujumbe huo ulimaanisha nini. ***(5: 5-9)***<br>3. Danieli aliletwa kama mtu pekee aliyeweza kufasiri maandishi ya ukutani. ***(5: 10-16)***<br>4. Danieli alieleza kwamba Mungu alikuwa akimwambia mfalme kwamba hakuwa amejifunza kutokana na yote yaliyompata baba yake. Hakuwa akimheshimu Mungu ambaye ameshikilia maisha yake na njia zake zote mkononi mwake! *Mungu anashikilia maisha yetu na njia zetu zote mkononi mwake, kama mfalme.* ***(5: 17-28)***<br>5. Mungu alimwadhibu Belshaza na akafa usiku huohuo, na ufalme wake ukagawanyika. Dario Mmedi akawa mtawala. ***(5: 30-31)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu**.<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Mkono wa ajabu. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Mfalme Belshaza alikuwa na karamu kubwa kwa wakuu wake 1,000. Alikuwa na kiburi na akachagua kupuuza masomo yote ambayo baba yake alikuwa amejifunza kuhusu kumfuata Mungu mmoja wa kweli. Alidai kutumia vikombe vya fedha na dhahabu kutoka katika Hekalu la Mungu huko Yerusalemu. ***(5: 1-2)***<br>2. Belshaza na marafiki zake hawakuonyesha heshima kwa Mungu na hazina za Hekaluni. Badala yake, waliabudu sanamu.<br>3. Vidole vya binadamu vilitokea ghafla na kuandika ujumbe ukutani. Mfalme aliogopa sana. Hakuna aliyeweza kusema ujumbe huo ulimaanisha nini. ***(5: 5-9)***<br>4. Danieli aliletwa kama mtu pekee aliyeweza kufasiri maandishi ya ukutani. ***(5: 10-16)***<br>5. Danieli alieleza kwamba Mungu alikuwa akimwambia mfalme kwamba hakuwa amejifunza kutokana na yote yaliyompata baba yake. Pia, kwamba Mungu hakupendezwa na maamuzi yake, mitazamo, na matendo yake.<br>6. Hakuwa akimheshimu Mungu ambaye ameshikilia maisha yake na njia zake zote mkononi mwake! *Mungu anashikilia maisha yetu na njia zetu zote mkononi mwake, kama mfalme.*(***5: 17-28)***<br>7. Mungu alimwadhibu Belshaza na akafa usiku huohuo, na ufalme wake ukagawanyika. Dario Mmedi akawa mtawala. ***(5: 30-31)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kusimama imara katika Mungu. |
| REJELEA SOMO | Tengeneza mchoro wa buibui kwa kutumia maandishi yanayonata ili kupendekeza jinsi Mungu anavyozungumza na watu leo. | Jadili katika vikundi vidogo, kisha mrejesho kwa kikundi kizima:<br>1. Ni nini kinachowafanya watu wampuuze Mungu?<br>2. Je, tunaweza kutarajia adhabu gani ikiwa tunampuuza Mungu? |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Je, Mungu bado anazungumza leo? Kwa njia zipi?<br>2. Je, tumempuuza Mungu na njia zake kama Belshaza?<br>3. Je, tunahitaji kuungama dhambi zetu na kumwomba Mungu msamaha? Soma ***Warumi 6: 23***. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Mungu anataka tumpe nafasi ya kwanza katika maisha yetu.<br>2. Tunaweza kufanya nini kitakachompendeza Mungu? Angalia katika ***Mathayo 6: 33, na Waebrania 11: 6***. |

| | C1 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Danieli<br>Mada – Tundu la simba | C1 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Danieli<br>Mada – Kuteseka kwa ajili ya Mungu |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Danieli 6: 1-28***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Danieli 6: 23***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Danieli alikuwa mwaminifu kwa Mungu licha ya mateso yote aliyokabiliana nayo.<br>2. Wakristo wanajua kwamba Mungu yuko pamoja nao sikuzote, licha ya magumu yoyote wanayopitia. | **Neno la Biblia:** ***Danieli 6: 1-28***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Danieli 6: 23***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Danieli alikuwa mwaminifu kwa Mungu licha ya mateso yote aliyokabiliana nayo.<br>2. Ni muhimu kumtanguliza Mungu maishani mwetu licha ya matukio yoyote ambayo tunaweza kupitia. |
| TOA UTANGULIZI | Fikiria mifano kutoka katika Biblia au historia ambapo mtu fulani alitetea yale aliyoamini na kuteseka kwa sababu hiyo. | Watu wanaomfuata Yesu wanaweza kupata upinzani wa aina gani? Ikiwezekana fanya utafiti - www.opendoorsuk.org |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Mfalme Dario sasa alitawala Babeli. Danieli alikuwa na jukumu kubwa la kutawala. Mfalme alimpenda Danieli na kumheshimu kwa sababu alifanikiwa sana katika kila jambo alilofanya. ***(6: 1-3)***<br>2. Wale wakuu wengine au maliwali walikuwa na wivu na wakapanga njama ya kumtia Danieli matatizoni. Walimshawishi Mfalme Dario kwamba kila mtu anapaswa kusujudu na kumwabudu yeye peke yake kwa siku 30. ***(6: 4-9)***<br>3. Kila siku Danieli aliendelea kwenda chumbani kwake na kumwomba Mungu mara tatu kwa siku. ***(6: 10)***<br>4. Hii iliripotiwa kwa mfalme. Alijaribu kupuuza amri yake mwenyewe, lakini hakuweza. Mfalme hakuwa na njia nyingine ila kumtupa Danieli katika tundu la simba. ***(6: 11-17)***<br>5. *Danieli alimwamini Mungu na alikuwa tayari kutanguliza muda wake wa kumwomba Mungu zaidi ya usalama wake mwenyewe. Danieli aliamini kwamba Mungu ndiye anayetawala na angeweza kumlinda katika tundu la simba.*<br>6. Mfalme alikosa usingizi usiku akiwa na wasiwasi juu ya Danieli, lakini alifurahi kumpata Danieli akiwa hai asubuhi iliyofuata. Mungu alikuwa amefunga vinywa vya simba! ***(6: 18-23)***<br>7. Wala njama hao walitupwa katika tundu la simba na kuliwa mara moja. ***(6: 24)***<br>8. Mfalme Dario aliamuru kwamba Mungu wa Danieli anapaswa kuheshimiwa na kutukuzwa. ***(6: 25- 26)*** *Eleza kwa maneno rahisi hii ina maana gani.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Tundu la simba. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Mfalme Dario sasa alitawala Babeli. Danieli alikuwa na jukumu kubwa la kutawala. Mfalme alimpenda Danieli na kumheshimu kwa sababu alifanikiwa sana katika kila jambo alilofanya. ***(6: 1-3)***<br>2. Wale wakuu wengine au maliwali walikuwa na wivu na wakapanga njama ya kumtia Danieli matatizoni. Walimshawishi Mfalme Dario kwamba kila mtu anapaswa kusujudu na kumwabudu yeye peke yake kwa siku 30. ***(6: 4-9)***<br>3. Kila siku Danieli aliendelea kwenda chumbani kwake na kumwomba Mungu mara tatu kwa siku. ***(6: 10)***<br>4. Hii iliripotiwa kwa mfalme. Alijaribu kupuuza amri yake mwenyewe, lakini hakuweza. Mfalme hakuwa na njia nyingine ila kumtupa Danieli katika tundu la simba. ***(6: 11-16)***<br>5. *Danieli alimwamini Mungu na alikuwa tayari kutanguliza muda wake wa kumwomba Mungu zaidi ya usalama wake mwenyewe. Danieli aliamini kwamba Mungu ndiye anayetawala na angeweza kumlinda katika tundu la simba.*<br>6. Mfalme alikosa usingizi usiku akiwa na wasiwasi juu ya Danieli, lakini alifurahi kumpata Danieli akiwa hai asubuhi iliyofuata. Mungu alikuwa amefunga vinywa vya simba! ***(6: 18-23)***<br>7. Wala njama hao walitupwa katika tundu la simba na kuliwa mara moja. ***(6: 24)***<br>8. Mfalme Dario aliamuru kwamba Mungu wa Danieli anapaswa kuheshimiwa na kutukuzwa. ***(6: 25- 26)*** *Eleza kwa maneno rahisi hii ina maana gani.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kuteseka kwa ajili ya Mungu. |
| REJELEA SOMO | Jadili katika vikundi vidogo, kisha fanya mrejesho kwa kikundi kizima:<br>Ni kwa njia gani Wakristo wangeweza kukosolewa kwa kumtetea Mungu shuleni?<br>Je, habari ya Danieli inatusaidiaje kujifunza jinsi ya kukabiliana na hili? | Jadili katika vikundi vidogo, kisha fanya mrejesho kwa kikundi kizima:<br>Hakuna mtu anapenda magumu. Mambo magumu ya Danieli yalimuathiri namna gani?<br>Tunapokabiliana na matatizo, mtazamo wetu unapaswa kuwaje? |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>Kwa nini tusiogope kumtetea Mungu?<br>Soma ***Yoshua 1: 9.***<br>Je, hii inamaanisha kuwa haitatokea wakabiliane na hali yoyote ngumu? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Danieli alikuwa na utaratibu wa kila siku wa kuomba mara 3 kwa siku. Ni masomo gani tunaweza kujifunza kutoka kwa yale ambayo yanaweza kuwa ya manufaa katika maisha yetu ya Kikristo?<br>2. Katika vikundi, fanyieni kazi aina ya sala ambayo huenda Danieli alisali kila mara alipoenda chumbani kwake. |

| | **C2 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Kwanza – Watu aliokutana nao Yesu**<br>**Mada – Yesu akutana na mtu huko Yeriko.** | **C2 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Kwanza – Maneno ya Yesu**<br>**Mada – Kuhusu dhambi** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Luka 19: 1-10***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 19: 10***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu alikutana na mtu aitwaye Zakayo - mtoza ushuru asiye na furaha, asiye mwaminifu.<br>2. Maisha ya Zakayo yalibadilika alipokutana na Yesu. | **Neno la Biblia:** ***Luka 19: 1-10***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 19: 10***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Kukutana na Yesu lilikuwa jambo la maana zaidi ambalo halikuwahi kutokea kwa Zakayo.<br>2. Zakayo hakubaki vile vile tena baada ya siku hiyo. Maisha yake yalibadilika. |
| **TOA UTANGULIZI** | Eleza kuhusu mchezo wa wakati mtu alipodanganya. Ulifanyaje kwa mtu ambaye alipuuza kanuni?<br>Somo la leo linahusu mtu ambaye hakuwa maarufu sana kwa sababu hakuwa mwaminifu. Watu walifikiri kuwa yeye ni mbaya, lakini Yesu alionyesha upendo kwake, na alitaka kukutana naye. | Zakayo hakuwa mtu maarufu.<br>Je, kuna watu wasio maarufu katika darasa au shule yako? Je, ni mambo gani yanafanya watu wasiwe maarufu?<br>Unaweza kuonyeshaje upendo kama Yesu alivyofanya kwa aina nyingi sana za watu? |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Zakayo alikuwa tajiri, lakini hakupendwa na watu wengi kwa sababu alifanya kazi kama mtoza ushuru wa Warumi. ***(19: 1-2)*** Wakati fulani hakuwa mwaminifu na alichukua pesa nyingi kuliko alizopaswa kutoza watu.<br>2. Zakayo alitaka kumwona Yesu alipokuja Yeriko na akapanda juu ya mti. Alifanya hivyo kwa sababu hakuwa mrefu sana! ***(19: 3-4)***<br>3. Yesu alimwomba Zakayo ashuke na kusema alitaka kwenda nyumbani kwa Zakayo. ***(19: 5-6)***<br>4. Zakayo alimkaribisha Yesu nyumbani kwake, lakini watu hawakufurahia jambo hilo.<br>5. Zakayo alijutia dhambi zake na akamwambia Yesu atatoa fedha zake awape maskini na watu aliowadanganya. ***(19: 8)***<br>6. Yesu alisema wokovu umekuja nyumbani kwa Zakayo. ***(19: 9)***<br>7. Yesu alisema amekuja kutafuta na kuokoa watu waliopotea kama Zakayo. Hii ni habari njema! ***(19: 10)*** *Eleza hilo linamaanisha nini kwa vijana leo.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Yesu akutana na mtu huko Yeriko. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Zakayo alikuwa tajiri, lakini hakupendwa na watu wengi kwa sababu alifanya kazi kama mtoza ushuru wa Warumi. ***(19: 1-2)*** Watu hawakuwaamini watoza ushuru na walimwona Zakayo kama msaliti. Wakati fulani hakuwa mwaminifu na alichukua pesa nyingi kuliko alizopaswa kutoza watu.<br>2. Zakayo alitaka kumwona Yesu alipokuja Yeriko na akapanda juu ya mti. Alifanya hivyo kwa sababu hakuwa mrefu sana! ***(19: 3-4)***<br>3. Yesu alijua Zakayo ni nani na alikuwa wapi. Alijua yote kuhusu Zakayo. Akamwomba Zakayo ashuke na kusema anataka kwenda nyumbani kwake. ***(19: 5-6)***<br>4. Zakayo alimkaribisha Yesu nyumbani kwake, lakini watu hawakufurahishwa sana na jambo hilo, kwa sababu Yesu alikuwa akienda kwenye nyumba ya mtu asiye maarufu sana.<br>5. Zakayo alijutia tabia yake ya dhambi na alitaka kuweka mambo sawa. Alijitolea kutoa pesa zake kwa maskini na kwa mtu yeyote ambaye alikuwa amemdanganya. ***(19: 8)***<br>6. Yesu alisema wokovu umekuja nyumbani kwa Zakayo. ***(19: 9)***<br>7. Yesu alisema amekuja kutafuta na kuokoa watu waliopotea kama Zakayo. Hii ni habari njema! ***(19: 10)***<br>8. *Tunapotubu, tunahitaji kujutia dhambi zetu lakini pia kuziacha na kuishi maisha yetu kwa ajili ya Mungu, kila inapowezekana tuweke mambo mabaya ambayo tumefanya kuwa sahihi. Tukimwomba, Bwana Yesu atatuokoa na kutusaidia kuishi maisha yetu kwa ajili ya Mungu.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kuhusu dhambi. |
| **REJELEA SOMO** | Mkiwa wawili wawili, wazeni kama mnafanya mahojiano na Zakayo kwa redio au televisheni kuhusu siku aliyokutana na Yesu na jinsi ilivyobadilisha maisha yake.Tayarisha baadhi ya maswali na majibu. Mtu mmoja anaweza kuwa mdadisi na mwingine anaweza kuwa Zakayo. Kumbuka kuweka msingi wa mahojiano yako kwenye habari katika ***Luke 19: 1-10.*** | Ukiwa peke yako au wawili wawili, jichukulie kama wewe ni Zakayo. Andika ingizo kwenye blogu kuhusu siku uliyokutana na Yesu na jinsi hali hiyo ilivyobadilisha maisha yako. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Je, watu wanapaswa kuwa wakamilifu au maarufu ili Mungu abadilishe maisha yao? Hapana! Zakayo hakuwa maarufu na alikuwa mwenye dhambi, lakini Yesu alimbadilisha.<br>2. Kwa kuwa Yesu alikuja kutafuta na kuokoa watu waliopotea, Wakristo wanapaswa kuwatendeaje watu 1) wasio maarufu? 2) wenye dhambi? 3) wasiomwamini Mungu? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Je! Kumfuata Yesu kunapaswa kuleta tofauti gani katika maisha yetu a) nyumbani, b) shuleni au chuoni, c) kanisani?<br>2. Kwa kufuata mfano wa Yesu, Wakristo wanapaswa kuwatendeaje watu wasio maarufu na watu wengine au wanaopuuza kanuni za Biblia? |

<table>
<tr>
<th></th>
<th>C2 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Pili – Watu aliokutana nao Yesu.<br>Mada – Yesu akutana na mwanamke kisimani.</th>
<th>C2 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Pili – Maneno ya Yesu<br>Mada – Kuhusu kuona</th>
</tr>
<tr>
<td></td>
<td>Neno la Biblia: Yohana 4: 5-30<br><br>Mstari Muhimu: Yohana 4: 29<br><br>Tunajifunza kuwa:<br>1. Yesu alikutana na mwanamke kisimani ambaye alidharauliwa na ambaye alikuwa mpweke.<br>2. Yesu anapenda, anajua, na anaweza kusaidia kila mtu.</td>
<td>Neno la Biblia: Yohana 9: 1-41<br><br>Mstari Muhimu: Yohana 9: 5<br><br>Tunajifunza kuwa:<br>1. Yesu alikutana na kipofu na kumponya.<br>2. Watu wasiomfuata Bwana Yesu ni vipofu kiroho. Yesu pekee ndiye anayeweza kuwapa uwezo wa kuijua kweli.</td>
</tr>
<tr>
<td>TOA UTANGULIZI</td>
<td>Jadili kuhusu kukimbia au matembezi marefu kwa muda mrefu siku ya joto. Je, ungekuwa na kiu? Ungejisikiaje kama mtu angekupa kinywaji? Tengeneza orodha ya vivumishi kuelezea jinsi ambavyo ungejisikia kupewa kinywaji baridi wakati ukiwa na kiu sana.</td>
<td>Maswali ya majadiliano ya kikundi:<br>• Je, wanawafahamu vipofu wowote?<br>• Maisha yao yakoje?<br>• Maisha yao yangebadilikaje kama wangeweza kuona ulimwengu unaowazunguka kwa ghafula?<br>• Watu wanaoona wanawezaje kuwasaidia wale walio vipofu?</td>
</tr>
<tr>
<td>KAMILISHA</td>
<td>Wasilisha Habari ya Biblia<br><br>Jadili na Uelezee:<br>1. Yesu aliposimama katika safari yake kupitia Samaria ili kupumzika kando ya kisima, alikutana na mwanamke Msamaria. (4: 4-7)<br>2. Wayahudi hawakuwapenda Wasamaria, na hawakuzungumza nao. Bwana Yesu alikuwa tofauti. Anampenda kila mtu hata awe nani. Mwanamke huyo alishangaa Yesu alipomwomba maji ya kunywa. Kwa kawaida, Wayahudi hawakuweza hata kuzungumza naye. (4: 7-9)<br>3. Yesu alipomwambia, angeweza kumpa maji ya uzima, alichanganyikiwa. (4: 10-14)<br>4. Yesu alijua yote kuhusu maisha na familia ya mwanamke Msamaria. Mwanamke huyu alitambua kuwa lazima alikuwa nabii. (4: 17-19)<br>5. Yesu alimwambia yule mwanamke kwamba Yeye ndiye Masihi ambaye watu wake walikuwa wakimngojea. (4: 26)<br>6. Mwanamke huyo alimwamini na akaenda mara moja kuwaambia marafiki zake na majirani katika mji huo. Aliacha mtungi wake wa maji kisimani. Alikuwa amegundua maji ya uzima ambayo Yesu pekee anaweza kutoa - uzima wa milele. (4: 28-30)<br>7. Eleza jinsi tunavyohitaji maji kimwili, lakini Yesu alikuwa akizungumza kuhusu uhitaji wetu wa kiroho wa maji ya uzima.<br><br>Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.<br>Kamilisha Somo la Pili.<br>Onesha: Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Yesu akutana na mwanamke kisimani.</td>
<td>Wasilisha Habari ya Biblia<br><br>Jadili na Uelezee:<br>1. Yesu alikutana na mtu aliyekuwa kipofu tangu kuzaliwa. Wanafunzi wake waliuliza kama upofu wake ulikuwa ni adhabu kutoka kwa Mungu. Yesu alisema kwamba angemponya mtu huyo ili kila mtu aweze kuona kazi za Mungu maishani mwake. (9: 1-3)<br>2. Yesu akampaka matope machoni na kumwambia aende akanawe katika Birika la Siloamu. Mwanamume huyo alimtii Yesu na akaweza kuona kimuujiza. (9: 6-7)<br>3. Mafarisayo waliambiwa juu ya muujiza huo na wakasema Yesu hangeweza kutoka kwa Mungu kwa sababu alikuwa ameponya siku ya Sabato. Hawakuamini kuwa Bwana Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. (9: 13-17)<br>4. Yule mtu aliyekuwa kipofu alianza kutambua kwamba ni Yesu aliyemfanya aone tena. Aliamini Bwana Yesu alikuwa Mwana wa Mungu na akamwabudu. (9: 35-38)<br>5. Kipofu aliweza kuona kimwili wakati Bwana Yesu alipomponya, lakini pia alitambua Yesu alikuwa nani na akamwamini. Kisha akaweza kuona kiroho na kimwili. Mafarisayo wangeweza kuona kimwili, lakini walikataa kuamini kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Walikuwa vipofu kiroho.<br>6. Bwana Yesu ni Nuru ya Ulimwengu. Alikuja ili tuweze kuwekwa huru kutoka katika upofu wa kiroho.<br><br>Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.<br>Kamilisha Funzo la Pili.<br>Onesha: Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kuhusu kuona.</td>
</tr>
<tr>
<td>REJELEA SOMO</td>
<td>1. Kwa kufuata mfano wa Yesu, tunapaswa kuwatendeaje watu wengine? Toa mifano.<br>2. Mwanamke alifanya nini Yesu alipomwambia kuwa yeye ndiye Masihi? Kwa nini? Matokeo ya kile alichokifanya yalikuwa nini?</td>
<td>Majadiliano ya wawili wawili: Soma kifungu cha Biblia tena na ujadili majibu baada ya muujiza kwa:<br>a) Majirani.<br>b) Wazazi wa kipofu.<br>c) Mafarisayo.<br>d) Mtu ambaye alikuwa kipofu.</td>
</tr>
<tr>
<td>LIISHI SOMO</td>
<td>Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?<br>1. Je, umepokea “maji yaliyo hai” ambayo Bwana Yesu anatoa? Je, umemwamini? Angalia Yohana 7: 37-39<br>2. Je, umewaambia watu wengine kuhusu Yesu?</td>
<td>Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?<br>Angalia Yohana 8: 12 na ufikirie jinsi tunavyoweza kujua “nuru ya uzima” katika maisha yetu.</td>
</tr>
</table>

| | C2 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Tatu – Watu aliokutana nao Yesu.<br>Mada – Yesu akutana na mtu usiku | C2 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Tatu – Maneno ya Yesu<br>Mada – Kuhusu wachungaji |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Yohana 3: 1-16***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 3: 16***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu alikutana na Nikodemo ambaye alikuwa Farisayo wa kidini lakini alitaka kusaidiwa.<br>2. Yesu alimwambia kuwa alihitaji kuzaliwa tena ili kupata karama ya Mungu ya maisha mapya. Tunapewa karama hii tunapomwamini Yesu. | **Neno la Biblia:** ***Yohana 10: 1-33***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 10: 9***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu alifundisha kwamba sisi ni kama kondoo na Yeye ni kama Mchungaji anayetutunza.<br>2. Tukimwamini, sisi tunakuwa kondoo wake na Yeye kama Mchungaji hatatuacha kamwe. |
| TOA UTANGULIZI | Zungumza na kikundi kuhusu kuzaliwa kwa mtoto mchanga. Kwa nini ni wakati wa kusisimua sana? Fikiria juu ya maisha mapya na umuhimu wa siku za kuzaliwa na faida zake. | Tengeneza orodha ya kazi ambazo wachungaji wanafanya (k.m. kulinda kondoo wao; kuongoza kondoo wao; kutafuta kondoo wanapopotea; kuwapa kondoo chakula na maji). |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Nikodemo alikuwa mtawala wa dini ya Kiyahudi aliyekuja kumwona Yesu usiku. Hatujui kwa nini. Labda aliona aibu kuja kumwona Yesu na akapendelea kuja kukiwa na giza.<br>2. Nikodemo alisema kwamba lazima Yesu alitoka kwa Mungu kwa sababu hakuna mtu angeweza kufanya miujiza ambayo Yesu alifanya bila msaada wa Mungu. ***(John 3: 1-2)***<br>3. Yesu alisema hakuna mtu anayeweza kuuona Ufalme wa Mungu asipozaliwa mara ya pili. Nikodemo hakuelewa jinsi mtu mzima angeweza kuzaliwa tena kama mtoto mchanga. ***(3: 3-4)***<br>4. Yesu alisema ili kuingia katika Ufalme wa Mungu watu wanahitaji kuzaliwa upya ili kupokea uzima wa Mungu, ambao hutolewa kwa Roho. ***(3: 5-8)***<br>5. Pia alimweleza Nikodemo kwamba angeinuliwa juu ya msalaba, kama vile nyoka wa shaba ambaye Musa alimwinua jangwani. Ikiwa wagonjwa walioumwa na nyoka walimtazama yule nyoka wa shaba, hawakufa bali waliponywa tena.***(Hesabu 21: 4-9) (Yohana 3: 14)***<br>6. *Alimwambia Nikodemo kwamba Mungu aliupenda ulimwengu sana hata akatupa Mwanawe, Yesu. Yesu aliinuliwa alipokufa msalabani. Yeyote anayemgeukia Yesu na kumwamini hatakufa bali atakuwa na uzima wa milele.* ***(Yohana 3: 16 - Mstari Muhimu)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Yesu akutana na mtu usiku. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Yesu aliwaambia Mafarisayo kwamba Yeye ni Mchungaji na, Yeye ni kama Lango la kondoo. Anatulinda kama vile mchungaji alindavyo lango la zizi la kondoo. ***(10: 7-11)*** Yesu alitumia mawazo haya kama mfano kujielezea zaidi kwa watu.<br>2. Yesu alisema kwamba tofauti na viongozi wengine, Yeye alikuja kuwapa watu uzima. ***(10: 10)***<br>3. Yesu alisema yeye ndiye Mchungaji Mwema ambaye alitoa maisha yake kwa ajili ya kondoo. ***(10: 11 & 14)***<br>4. Baadhi ya watu walifikiri Yesu alikuwa mwendawazimu. Wengine walikataa kuamini kuwa yeye ni Mwana wa Mungu. ***(10: 21 & 24-25)***<br>5. Yesu aliwaambia Wayahudi kwamba mambo makuu aliyokuwa akifanya yalionyesha kwamba alikuwa Masihi aliyetoka kwa Mungu. Waliposikia haya, baadhi ya Wayahudi walikataa kumwamini. Walijaribu kumuua Yesu kwa kumpiga mawe. Watu hawa hawakuwa kondoo Wake. ***(10: 31-33)***<br>6. Hata hivyo, baadhi ya watu walimwamini Yesu. Watu hawa walikuwa kondoo wake.<br>7. Tukiachwa peke yetu, tunatangatanga mbali na Mungu. Tunamhitaji Bwana Yesu atuongoze katika njia tunayopaswa kuiendea na kutupa uzima wa milele. ***(10: 28) (Angalia Isaya 53: 6)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kuhusu wachungaji. |
| REJELEA SOMO | Maswali:<br>1. Yesu alisema nini kilipaswa kutokea kabla mtu hajaona Ufalme wa Mungu?<br>2. Je, Yesu alisema kwamba Nikodemo angepaswa kuwa mtoto tena?<br>3. Je, tunapaswa kulipia maisha mapya ya Mungu?<br>4. Ni nini kilifanyika wakati watu ambao ni wagonjwa walipomtazama nyoka wa shaba aliyeinuliwa na Musa kule jangwani? Nini kilifanyika walipoacha kufanya hivyo?<br>5. Tunapaswa kufanya nini ili kupokea karama ya Mungu ya uzima wa milele?<br>6. Nini kitatokea tukimwamini Yesu? | Majadiliano ya kikundi: Yesu alimaanisha nini aliposema kuwa alikuwa:<br>1. Lango la kondoo? ***(10: 9)***<br>2. Mchungaji Mwema? ***(10: 11 & 14)*** |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>Je, umemwomba Bwana Yesu akupe maisha mapya ya Mungu? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>Angalia orodha ya kazi zinazofanywa na wachungaji.<br>Je, tunapata tofauti gani tunapomjua Yesu kama Mchungaji wetu? |

| | **C2 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Nne – Watu aliokutana nao Yesu**<br>**Mada – Yesu akutana na kipofu.** | **C2 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Nne – Maneno ya Yesu**<br>**Mada – Kuhusu wokovu** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Yohana 9: 1-38***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 9: 25***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu alikutana na kumponya kipofu.<br>2. Watu wasiomfuata Bwana Yesu ni vipofu kiroho. Yesu pekee ndiye anayeweza kuwapa uwezo wa kujua kweli. | **Neno la Biblia:** ***Yohana 3: 1-16***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 3: 16***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu alikutana na Nikodemo ambaye alikuwa Farisayo wa kidini lakini alitaka kusaidiwa.<br>2. Yesu alimwambia alihitaji kuzaliwa tena ili kupata karama ya Mungu ya uzima mpya. Huu uzima unatolewa kwetu tunapomwamini Yesu. |
| **TOA UTANGULIZI** | Jadili kuhusu kukutana na kipofu. Ni changamoto zipi zinazowakabili watu wasioona? Mkiwa wawili wawili, tengenezeni orodha ya hizo changamoto na linganisha na kundi zima. Fikiria pia jinsi mtu anayeona anavyoweza kumsaidia kipofu. | Majadiliano ya kikundi au wawili wawili: Kuzaliwa kwa mtoto mchanga ni wakati wa kusisimua. Kwa nini? Fikiria juu ya maisha mapya na umuhimu wa siku za kuzaliwa na umuhimu wake. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Yesu alikutana na mtu aliyekuwa kipofu tangu kuzaliwa. Wanafunzi wake waliuliza kama upofu wake ulikuwa ni adhabu kutoka kwa Mungu. Yesu alisema kwamba angemponya mtu huyo ili kila mtu aweze kuona kazi za Mungu katika maisha Yake. ***(9: 1-3)***<br>2. Yesu akampaka tope za macho na kumwambia akanawe katika Birika ya Siloamu. Mwanamume huyo alimtii Yesu na akaweza kuona kimuujiza. ***(9: 6-7)***<br>3. Mafarisayo waliambiwa kuhusu muujiza huo na wakasema Yesu hangeweza kutoka kwa Mungu kwa sababu alimponya kipofu siku ya Sabato. Hawakuamini kuwa Bwana Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Yule kipofu alisema kwamba anadhani Yesu alikuwa nabii. ***(9: 13-17)***<br>4. Yule mtu aliyekuwa kipofu alitambua kwamba ni Yesu aliyemfanya aone tena. Aliamini Bwana Yesu alikuwa Mwana wa Mungu na akamwabudu. ***(9: 35-38)***<br>5. *Kipofu aliweza kuona kimwili wakati Bwana Yesu alipomponya, lakini pia alitambua Yesu alikuwa nani na alimwamini. Kisha aliweza kuona kiroho na kimwili. Mafarisayo wangeweza kuona kimwili, lakini walikataa kuamini kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu. Walikuwa vipofu kiroho.*<br>6. *Bwana Yesu ni Nuru ya Ulimwengu. Alikuja ili tuweze kuwekwa huru kutoka katika upofu wa kiroho.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Yesu akutana na kipofu. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Nikodemo alikuwa mkuu wa dini ya Kiyahudi aliyekuja kumwona Yesu usiku. Hatujui kwa nini. Labda alitaka mazungumzo hayo yafanyike kwa siri.<br>2. Nikodemo alisema lazima Yesu alitoka kwa Mungu kwa sababu hakuna mtu angeweza kufanya miujiza ambayo Yesu alifanya bila msaada wa Mungu ***(Yohana 3: 1-2)***<br>3. Yesu alisema hakuna mtu anayeweza kuuona Ufalme wa Mungu isipokuwa amezaliwa mara ya pili. Nikodemo hakuelewa jinsi ambavyo mtu mzima angeweza kuzaliwa tena kama mtoto mchanga. ***(3: 4)*** Yesu alieleza kwamba kuzaliwa mara ya pili alikokuwa akieleza kulikuwa kwa kiroho badala ya kimwili.<br>4. Yesu alisema ili kuingia katika Ufalme wa Mungu, watu wanahitaji kuzaliwa tena ili wapate karama ya Mungu ya uzima mpya. Huu uzima unatolewa na Roho Mtakatifu. ***(3: 5-8)***<br>5. Yesu pia alimweleza Nikodemo kwamba angeinuliwa juu ya msalaba, kama ilivyokuwa kwa nyoka wa shaba ambaye Musa alimuinua jangwani. Wagonjwa walioumwa na nyoka walipomtazama yule nyoka wa shaba, hawakufa bali waliponywa. ***(Hesabu 21: 4-9) (Yohana 3: 14)***<br>6. Yesu alimwambia Nikodemo kwamba Mungu aliupenda ulimwengu hata akatupa Mwanawe, Yesu. Yesu aliinuliwa alipokufa msalabani. Yeyote anayemgeukia Yesu na kumwamini hatakufa bali atakuwa na uzima wa milele. ***(Yohana 3: 16 - Mstari Muhimu)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho A – Kuhusu wokovu. |
| **REJELEA SOMO** | Tengeneza ubao wa hadithi wa kuchekesha wa matukio katika habari ya leo. Vinginevyo, ubao mkubwa zaidi unaweza kukamilishwa na wawiliwawili na kubandikwa ukutani. | Majadiliano ya kikundi:<br>1. Je, mazungumzo ambayo Nikodemo alikuwa nayo na Bwana Yesu yanatufundisha nini kuhusu kuwa Mkristo?<br>2. Tunapomwamini Yesu maisha yetu yanakuwa na tofauti gani? |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Je, watu wafuatao walitofautiana vipi katika mitazamo yao? a) Kipofu b) Mafarisayo, c) majirani d) wazazi wake?<br>2. Fikiria kuhusu mwitikio wako binafsi kwa Bwana Yesu. Je, uko tayari, kama yule kipofu, kuweka imani yako Kwake? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Je, umemwamini Yesu kwa ajili ya uzima wa milele?<br>2. Je, umezaliwa mara ya pili? |

| | C3 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Kwanza – Miujiza zaidi<br>Mada – Yesu amsaidia mgonjwa | C3 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Kwanza – Kuponya wagonjwa<br>Mada – Nguvu za Bwana |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Yohana 5: 1-16***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 5: 9***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu alikutana na mwanamume aliyekuwa mgonjwa kwa miaka mingi.<br>2. Mtu huyo hakuweza kujiponya mwenyewe. Yesu pekee ndiye aliweza kufanya hivyo. | **Neno la Biblia:** ***Yohana 5: 1-16***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 5: 24***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu ni mwenye nguvu na fadhili. Ana rehema na huwabariki watu wanapomwamini, si kwa sababu ya kutii sheria fulani.<br>2. Ni muhimu zaidi kumwamini Mungu na kumwamini Bwana Yesu kuliko kufuata kanuni na taratibu za kidini. |
| TOA UTANGULIZI | Mwanaume katika habari ya leo alikuwa akingoja kuponywa kwa miaka 38. Hesabu kuna siku ngapi katika miaka 38. Chunguza baadhi ya mambo yaliyotokea au kuchukua nafasi miaka 38 iliyopita ili kupata wazo fulani la urefu huu wa muda. | Katika hadithi hii, Wayahudi walimtesa Bwana Yesu kwa kutofanya mambo kwa jinsi walivyofikiri angetakiwa kufanya. Njia za Mungu zinaweza kuonekana tofauti na njia zetu, lakini tunahitaji kumtii badala ya kufuata mawazo yetu wenyewe. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Yesu alipokuwa hapa, watu wengi walikuwa wamelala kando ya birika huko Yerusalemu liitwalo Bethzatha. Walikuwa na matumaini ya kuponywa wakati maji yalipotibuliwa. ***(5: 1-3)***<br>2. Siku moja ya Sabato, Yesu alimwona mwanaume aliyekuwa amengojea huko kwa miaka 38! Yesu alimuuliza kama alitaka kupona. ***(5: 5-6)***<br>3. Mwanaume huyo alieleza kwamba hakuwa na mtu wa kumsaidia kuingia kwenye birika hilo ili apone. Kila wakati mtu mwingine alimtangulia. Yesu alimwambia mtu huyo ainuke, achukue godoro lake na aende. Mtu huyo aliamka mara moja. Yesu alikuwa amemponya mtu huyo! ***(5: 7-9)***<br>4. Mtu huyo hakujua ni nani aliyemfanya kuwa mzima. Baadaye, Yesu alimwona mtu huyo tena Hekaluni. Yule mtu alipotambua ni nani aliyemponya, akaenda kuwaambia watu ni Yesu ndiye aliyemponya. ***(5: 14-15)***<br>5. Wayahudi walimtesa Yesu kwa sababu alimponya mtu siku ya Sabato. Waliamini kwamba hakuna kazi yoyote iliyopaswa kufanywa siku ya Sabato. Hawakuelewa au kukubali kwamba Yesu alikuwa akifanya kazi ya Mungu. ***(5: 16)***<br>6. *Eleza kwamba Yesu hakuponya watu siku hizo tu bali sasa Anaweza pia kuwaokoa wote wanaomjia na kumtumaini.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Yesu amsaidia mgonjwa. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Yesu alipokuwa hapa, watu wengi walikuwa wamelala kando ya birika huko Yerusalemu liitwalo Bethzatha. Walikuwa na matumaini ya kuponywa wakati maji yalipotibuliwa. ***(5: 1-3)***<br>2. Siku moja ya Sabato, Yesu alimwona mwanaume aliyekuwa amengojea huko kwa miaka 38! Yesu alimuuliza kama alitaka kupona. ***(5: 5-6)***<br>3. Mwanamume huyo alieleza kwamba hakuwa na mtu wa kumsaidia kuingia kwenye birika hilo ili apone. Kila wakati mtu mwingine alimtangulia. Yesu alimwambia mtu huyo ainuke, achukue godoro lake na atembee. Mtu huyo aliamka mara moja. Yesu alikuwa amemponya mtu huyo! ***(5: 7-9)***<br>4. Mtu huyo hakujua ni nani aliyemfanya kuwa mzima. Baadaye, Yesu alimwona mtu huyo tena Hekaluni. Yule mtu alipotambua ni nani aliyemponya, akaenda kuwaambia watu ni Yesu ndiye aliyemponya. ***(5: 14-15)***<br>5. Wayahudi walimtesa Yesu kwa sababu alimponya mtu siku ya Sabato. Waliamini kwamba hakuna kazi yoyote iliyopaswa kufanywa siku ya Sabato. Hawakuelewa au kukubali kwamba Yesu alikuwa akifanya kazi ya Mungu. ***(5: 16)***<br>6. *Eleza kwamba Yesu hakuponya watu siku hizo tu bali sasa Anaweza pia kuwaokoa wote wanaomjia na kumtumaini.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kuponya wagonjwa. |
| REJELEA SOMO | Watoto wangeweza kuandika makala fupi ya gazeti kuhusu matukio yaliyotokea katika habari ya leo. Wanapaswa kufikiria kichwa cha habari kinachofaa kwa makala zao. Unaweza kutengeneza onyesho la ukuta na nakala zinazotolewa na darasa. | Andika maelezo mawili mafupi: moja kuhusu mtu aliyeponywa, na lingine kuhusu Wayahudi ambao hawakukubali kitendo cha Bwana Yesu cha kumponya mtu siku ya Sabato. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Yesu alimsaidia mtu mwenye uhitaji. Je, tunawezaje kuwasaidia wengine wenye uhitaji?<br>2. Bwana Yesu anaweza kutuokoa mara moja ikiwa tutamwamini na kuweka tumaini letu kwake. Angalia ***Matendo 16: 31*** na uone umuhimu kwa kila mtu. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Tafakari juu ya mitazamo tofauti kwa Bwana Yesu katika habari hii.<br>2. Je, umeweka tumaini lako Kwake au unapendelea kujaribu kumpendeza Mungu kwa kushika sheria fulani?<br>3. Kulingana na habari hii, njia ya Mungu ni ipi? |

| | C3 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Pili – Miujiza zaidi<br>Mada – Yesu amsaidia mtu mwenye huzuni | C3 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Pili – Kufufua wafu<br>Mada – Nguvu za Bwana |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Marko 5: 21-43***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Marko 5: 42***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu alikutana na mwanaume ambaye binti yake alikuwa mgonjwa sana na hakuna mtu mwingine aliyeweza kumsaidia.<br>2. Yesu alithibitisha kuwa hakuwa na uwezo juu ya magonjwa tu bali pia juu ya kifo. | **Neno la Biblia:** ***Luka 8: 40-56***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 11: 25***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu alikutana na mwanaume ambaye binti yake alikuwa mgonjwa sana na hakuna mtu mwingine aliyeweza kumsaidia.<br>2. Yesu alithibitisha kuwa hakuwa na uwezo juu ya magonjwa tu bali pia, juu ya kifo. |
| TOA UTANGULIZI | Elezea historia ya habari hii. Yairo alikuwa kiongozi wa sinagogi la mahali hapo, ambapo Wayahudi walikutana kuabudu wakati waliposhindwa kwenda kwenye Hekalu la Yerusalemu. Angekuwa na jukumu la ibada, kuendesha shule ya kila wiki na kutunza jengo. Viongozi wengi wa sinagogi walikuwa na uhusiano wa karibu na Mafarisayo waliotaka kumuua Yesu. Alikuja kwa Yesu kwa sababu alitamani sana msaada. | Elezea hstoria ya habari hii. Yairo alikuwa kiongozi wa sinagogi la mahali hapo. Viongozi wengi wa sinagogi walikuwa na uhusiano wa karibu na Mafarisayo waliotaka kumuua Yesu. Alikuja kwa Yesu kwa sababu alitamani sana kuwasaidia watu kama vile mwanamke aliyekuwa na magonjwa yasiyopona ambao Marabi waliwaona kuwa najisi. Jamii iliwaepuka lakini Yesu aliwafikia na kuwasaidia. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Yairo alimjia Yesu na kumsihi aje kumponya binti yake. Yesu alijibu mara moja na kuanza safari kwenda nyumbani kwa Yairo. ***(5: 22-24)***<br>2. Akiwa njiani kuelekea nyumbani kwa msichana huyo, Yesu alicheleweshwa na mwanamke aliyekuwa mgonjwa kwa miaka 12 na hakuna daktari aliyeweza kumponya. ***(5: 25-26)*** Kwa imani, aligusa vazi Lake na kuponywa. Yesu alimfanya akiri hadharani yale yaliyotukia. ***(5: 27-34)*** Yesu hakumkasirikia, bali aliipongeza imani yake, na kumwambia aende nyumbani kwa amani.<br>3. Yesu alipokuwa akiendelea kwenda nyumbani kwa Yairo, Yairo alipata ujumbe kwamba binti yake amekufa, lakini Yesu akamtia moyo asiogope bali aamini. ***(5: 35-36)*** Yesu alipofika nyumbani kwa Yairo, kulikuwa na waombolezaji wengi, lakini Yesu akawatoa nje wote.<br>4. Akiwa na wanafunzi watatu tu na wazazi wa msichana huyo, Yesu alimfufua msichana huyo akawa hai tena. Walishangaa sana aliposimama, kutembea, na kula chakula! Yesu pekee ndiye angeweza kumfanya awe hai tena! ***(5: 41-43)***<br>5. *Yesu alionyesha uwezo Wake mkuu juu ya ugonjwa alipomponya mwanamke ambaye alikuwa amekutana naye barabarani na uwezo Wake mkuu juu ya kifo alipomfufua msichana huyo.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Yesu akutana na kipofu. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Lilikuwa jambo lisilo la kawaida kwa kiongozi wa sinagogi anayeheshimika, kama Yairo, kuanguka miguuni pa Yesu na kumwomba amponye binti yake! ***(Luka 8: 40-42)***<br>2. Akiwa njiani kuelekea nyumbani kwa Yairo, Yesu alicheleweshwa na mwanamke aliyekuwa mgonjwa kwa miaka kumi na miwili. Yesu alijua kwamba mwanamke huyo alikuwa amemgusa kimakusudi lakini alitaka kumfundisha kwamba halikuwa vazi lake, bali imani yake katika Yeye ndiyo ilimponya. Pia alitaka kufundisha umati wa Wayahudi somo kuhusu kitendo chao cha kumtenga katika hali yake ya kusikitisha. Yesu hakumkasirikia, bali aliipongeza imani yake, na kumwambia aende nyumbani kwa amani. ***(8: 43-48)***<br>3. Yesu alipokuwa akienda nyumbani kwa Yairo, Yairo alipata ujumbe kwamba binti yake alikuwa amekufa. Yesu alimwambia Yairo asiogope bali aamini na akaenda nyumbani kwake. ***(8: 49-50)*** Yesu alipofika nyumbani kwa Yairo, kulikuwa na waombolezaji wengi huko, lakini Yesu akawatoa wote nje.<br>4. Akiwa na wanafunzi watatu tu na wazazi wa msichana huyo, Yesu alimfufua msichana huyo akawa hai tena. Walishangaa sana aliposimama, kutembea, na kula chakula! Yesu pekee ndiye aliweza kumfanya awe hai tena! ***(8: 51-56)***<br>5. *Yesu alionyesha uwezo wake mkuu juu ya ugonjwa alipomponya mwanamke ambaye alikuwa amekutana naye barabarani na uwezo wake mkuu juu ya kifo alipomfufua msichana huyo.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kufufua wafu. |
| REJELEA SOMO | Pitia kwa kujadili wahusika wanne katika habari:<br>1. Baba wa Msichana – alishikilia nafasi gani? Kwa nini alikuja kwa Yesu? Je, alikutana na kikwazo gani?<br>2. Yesu - huruma na faraja yake.<br>3. Msichana - Hali ya kusikitisha, kufa akiwa na umri wa miaka 12.<br>4. Wenye dhihaka - Jinsi ilivyokuwa vibaya kumdhihaki Bwana Yesu. | Umeombwa uandike makala kwenye gazeti la Habari za Galilaya, kuhusu binti wa Yairo kufufuliwa na mwanamke huyo kuponywa. Jadilini mkiwa wawili wawili, na mripoti kwenye kikundi Makala hiyo inapaswa kuwa na maelezo gani. Hakikisha unasisitiza kwamba Yesu aliweza kufufuka kutoka kwa wafu kwa sababu alikuwa Mungu. ***(Warumi 1: 4)*** |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>Tunapoweka imani yetu katika Bwana Yesu, Yeye hubadilisha maisha yetu milele. Ana uwezo juu ya uzima na kifo. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>Wakati wa shida fanya kile ambacho Yairo alikifanya - weka imani yako katika Bwana Yesu na uamini ahadi ambazo ametoa katika Biblia kwa wale ambao ni watu Wake. |

| | C3 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Tatu – Miujiza zaidi<br>Mada – Yesu amsaidia mtumwa wa akida | C3 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Tatu – Kusaidia wahitaji<br>Mada – Nguvu za Bwana |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Luka 7: 1-10***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 7: 9***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu alikutana na akida ambaye mtumishi wake alikuwa mgonjwa sana.<br>2. Imani ya akida katika maneno na kazi za Yesu ni mfano kwa kila mtu. | **Neno la Biblia:** ***Mathayo 8: 1-13***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 8: 13***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu anawasaidia watu wawili zaidi, ambao wote wawili walionyesha imani kubwa Kwake.<br>2. Yesu anaonyesha upendo na msaada wake kwa kila mtu bila kujali ni nani. |
| TOA UTANGULIZI | Elezea hostoria ya habari hii. Warumi walikuwa wamechukua nchi; akida (asiye Myahudi) labda alikuwa msimamizi wa watu 100 katika kituo cha Kapernaumu. Wazee wa Kiyahudi walikuja kwa Yesu kumwomba amponye mtumishi wa akida. Ilikuwa nafasi ya ajabu kwao kwa kuwa hawakumwamini Yesu, lakini walikuwa wameombwa kumkaribia Yesu. | Waulize wanafunzi kufikiria makundi mbalimbali ya watu ambayo yametengwa katika jamii yetu na mara nyingi hudharauliwa na kukataliwa. Wakumbushe kwamba katika siku za Yesu, watu waliokuwa na ukoma na watumwa mara nyingi walipuuzwa na kukataliwa. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Akida alikuwa amesikia juu ya nguvu za Yesu za kuponya. Alikuwa mwema sana kwa Wayahudi na hata akawajengea sinagogi na hivyo wazee wa Kiyahudi walitii ombi lake na wakaja kwa Yesu. ***(7: 1-4)***<br>2. Walimwambia Yesu kwamba yule akida Mmataifa alikuwa mtu mwema, kwa hiyo Yesu akaondoka kwenda kwenye nyumba ya yule akida. ***(7: 5-6)***<br>3. Yule akida hakujiona kuwa anastahili Yesu kuingia nyumbani kwake au kuja kwake. Alituma marafiki kwa Yesu na ujumbe. Hata hivyo, aliamini kwamba Yesu angeweza kumponya mtumwa wake bila kuwa pale ana kwa ana. Neno kutoka Kwake lingemponya mtumishi. Alitambua kwamba kama vile alivyokuwa chini ya mamlaka ya Serikali ya Kirumi na askari wake walivyokuwa chini ya mamlaka yake, Yesu alikuwa na aina hiyo hiyo ya mamlaka juu ya magonjwa. ***(7: 6-8)***<br>4. Yesu alistaajabia imani ya yule akida kwani hakuna Myahudi hata mmoja aliyekubali kwamba Yesu alikuwa na mamlaka kamili hivyo walipaswa kujua zaidi! ***(7: 9-10)***<br>5. *Katika **Marko 6: 6**, Yesu alistaajabia kutokuamini kwa Wayahudi! Imani kubwa ya akida ilipata thawabu pale mtumishi alipoponywa. Imani yake kwa Yesu ni mfano kwa kila mtu.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu**.<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Yesu amsaidia mtumishi wa askari. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Ukoma ulikuwa ugonjwa wa kutisha ambao haukuwa na tiba na kwa ujumla kuhani alimfukuza mtu mwenye ukoma kutoka nyumbani kwake, ili kuishi na jumuiya ya wakoma wengine, mpaka apate nafuu au kufa.<br>2. Yule mtu mwenye ukoma alikuja akimsihi Yesu amsaidie.<br>3. Yesu alipoonyesha upendo kwa mtu huyo, alinyoosha mkono akamgusa mtu huyo mwenye ukoma, akapona. Sheria ilitaka mwenye ukoma aliyeponywa achunguzwe na kuhani na hivyo Yesu akamtuma kwa kuhani kuthibitisha ukoma wake umeondoka na ili aweze kurudi nyumbani. ***(8: 1-4)***<br>4. Yule akida pia alimwendea Yesu akiomba msaada kwa ajili ya mtumishi wake. Yesu aliahidi kuja nyumbani kwake. Akida alionyesha heshima na unyenyekevu wake kwa kusema hakustahili Yesu aje nyumbani kwake.<br>5. Imani ya akida wa Kirumi, mtu wa Mataifa, inatofautiana sana na ile ya Wayahudi. Katika tendo lisilo la kawaida la upendo na huruma, alimwomba Yesu amponye mmoja wa watumishi wake. Aliamini Yesu angeweza kuponya hata akiwa mbali. ***(8: 5-9)***<br>6. Imani ya kweli ya akida ilimshangaza Yesu - kwa hakika, imani ya Mmataifa huyu iliwaaibisha viongozi wengi wa dini ya Kiyahudi wa siku hizo. Yesu aliipa thawabu imani ya yule akida, na mtumishi wake akaponywa mara moja! ***(8: 10-13)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kusaidia wahitaji. |
| REJELEA SOMO | Pitia somo kwa kujadili yafuatayo:<br>• Ombi la akida lilikuwa nini?<br>• Mtumishi wake alipata shida gani?<br>• Yesu aliionaje imani ya akida?<br>• Yesu alisema nini kuhusu imani yake?<br>• Andiko la ***Waebrania 11: 6*** linasema tunapaswa kuwa na nini kabla ya kumpendeza Mungu? | 1. Linganisha uponyaji wa mtumishi wa akida katika habari hii na ***Luka 7: 1-10***. Jadili tofauti na mfanano.<br>2. Linganisha jinsi Yesu alivyomponya mwenye ukoma katika habari hii na utakaso wa wenye ukoma katika ***Luka 17: 11-19.***<br>3. Ni nini kilikushangaza kuhusu habari hii? |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Kama vile akida alivyokuwa akijali mtumishi wake, vivyo hivyo Wakristo wanapaswa kujali kuwaleta wengine kwa Yesu.<br>2. Daima kumbuka kwamba Bwana Yesu ana mamlaka ya mwisho duniani na Mbinguni, bila kujali wengine wanaweza kusema nini. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Mguso wa uponyaji wa Kristo pekee ndio unaweza kuondoa ugonjwa wa dhambi na kutufanya tustahili kumwabudu Bwana Yesu.<br>2. Bwana Yesu alifurahishwa na imani ya yule akida. Ikiwa unamwamini Yesu, uwe na lengo la kumpendeza pia. Ukifanya hivyo, atakuheshimu na kukubariki. |

| | C3 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Miujiza zaidi<br>Mada – Yesu asaidia umati wenye njaa. | C3 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Kulisha wenye njaa<br>Mada – Nguvu za Bwana |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Yohana 6: 1-15***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 6: 35***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu alionyesha nguvu zake kwa kulisha umati mkubwa wa watu.<br>2. Yesu anaweza kukidhi mahitaji ya wote wanaokuja kwake na kumwamini. | **Neno la Biblia:** ***Yohana 6: 1-15***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 6: 35***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Muujiza huu ulikuwa ishara nyingine katika Injili ya Yohana kuthibitisha kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu kweli.<br>2. Tunaweza kumwamini Yesu atupatie mahitaji yetu ya kila siku ya kimwili na kiroho. |
| **TOA UTANGULIZI** | Soma mistari sita ya kwanza ya usomaji wa Biblia. Kisha anza kwa kuwazia jinsi ambavyo ingekuwa vigumu kulisha umati mkubwa kiasi hicho porini. Fikiria matatizo ambayo wanafunzi walikabiliana nayo Yesu alipowaambia waandae chakula kwa ajili ya umati wa watu. | Muujiza huo ni wa pekee kwa sababu ndio pekee uliorekodiwa na waandikaji wanne wa Injili. Pia ni muujiza pekee ambapo umati mkubwa ulipokea baraka. Wakumbushe wanafunzi kwamba Yesu ana upendo kwa kila mtu na anataka kila mtu amwamini na kumfuata. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Bwana Yesu alipoona umati mkubwa, katika tukio hili, wazo lake la kwanza lilikuwa kuwapa chakula. Alimuuliza Filipo mkate ungeweza kununuliwa wapi lakini Filipo alifikiria juu ya gharama na sio ukweli kwamba Yesu alikuwa na uwezo wa kulisha kila mtu. ***(6: 1-7)***<br>2. Ingawa Andrea pia alifikiri ingekuwa vigumu kuulisha umati, anataja mvulana huyo mwenye mikate mitano na samaki wawili. Ingawa hakuwa na vingi, kijana huyo alimpa Yesu vyote alivyokuwa navyo. ***(6: 8-9)***<br>3. Baada ya kutoa shukrani, Yesu aliwapa wanafunzi chakula wawagawie watu. Watu walikula walivyotaka na Yesu akawaagiza wanafunzi wake wakusanye mabaki, akitufundisha kwamba kusiwe na upotevu wa vitu anavyotupatia siku baada ya siku. ***(6: 10-13)***<br>4. *Yesu alitumia muujiza huu kueleza kwamba "Yeye alikuwa mkate wa uzima" ambaye hutupatia uzima wa milele ili tutosheke kiroho. (angalia Mstari Muhimu)*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Yesu asaidia umati wenye njaa. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Yesu alikuwa amesafiri kutoka Yerusalemu hadi ufukwe wa kaskazini wa Bahari ya Galilaya na umati mkubwa wa watu ulimfuata, labda kwa sababu waliona miujiza Aliyokuwa amefanya. Umati huu ulikuwa kama 'kondoo wasio na mchungaji' ***(Marko 6: 34)*** na hivyo Yesu akawahurumia.<br>2. Imani ya wanafunzi ilikuwa dhaifu lilipokuja swala la kulisha umati. Filipo alifikiria juu ya gharama na si juu ya ukweli kwamba Yesu alikuwa na uwezo wa kulisha kila mtu. Andrea aliona mvulana mmoja akiwa na mikate mitano na samaki wawili lakini akauliza chakula hicho kidogo kingesaidia nini kwa idadi kubwa ya watu kiasi kile. ***(6: 1-9)***<br>3. Yesu aliwaketisha watu wote, na baada ya kushukuru, akaizidisha mikate na samaki na akawapa wanafunzi chakula, waugawie umati. ***(6: 10-11)***<br>4. Hakukuwa na uhaba wa chakula pamoja na kuambiwa watu walishiba, tunaambiwa jinsi Bwana Yesu alivyowaagiza wanafunzi wakusanye katika vipande vilivyobaki! Muujiza mkubwa ulikuwa umefanyika! ***(6: 12-13)***<br>5. Umati huo ulitambua kuwa ulikuwa ni muujiza na hata kukiri kwamba Yesu alikuwa nabii aliyetabiriwa katika ***Kumbukumbu la Torati 18: 15***. Hata hivyo, imani yao haikuwa ya kweli, na hawakuwa tayari kukiri kwamba Yesu alikuwa Mwana wa Mungu au kuungama dhambi zao na kumkubali kama Mwana wa Mungu na Mwokozi wao.<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kulisha wenye njaa. |
| **REJELEA SOMO** | Rudia somo kwa kuwauliza watoto kufikiria habari hii iliyosimuliwa katika gazeti la mtaa wao. Mwandishi wa habari anaweza kusema nini kuhusu:<br>(i) Hali ya umati?<br>(ii) Wema wa Bwana Yesu?<br>(iii) Maswali ya wanafunzi?<br>(iv) Utoaji wa Bwana Yesu?<br>(v) Mtazamo wa Bwana Yesu kuhusu uharibifu wa chakula? | Gawa Masomo haya ya Biblia katika vikundi 3.<br>***Mathayo 14: 13-21, Marko 6: 33-44, Luka 9: 10-17***<br><br>Zungumzia kile ambacho kila kikundi kilijifunza kutokana na simulizi iliyosomwa na kikundi chao ambayo haikuwa katika Injili ya Yohana. Vikundi vyote vitatu vinaripoti na kushirikisha utafiti wao. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Mstari Muhimu unatuambia kwamba tunahitaji kuja kwa Yesu, ambaye ni Mkate wa Uzima, ambaye anaweza kutosheleza utupu ulio ndani yetu.<br>2. Yesu anahitaji vijana wamtumikie. Kama vile mvulana mdogo alivyofanya. Alichotoa kilimwezesha Yesu kufanya muujiza wa ajabu. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Kama unamwamini Yesu, atakidhi mahitaji yako ya kila siku ya kimwili na kiroho.<br>2. Kama Yesu alivyozidisha mikate mitano na samaki wawili, Anaweza kutumia na kuzidisha chochote tunachompa ikiwa sisi ni watu wake. Hii inaweza kuwa vipaji vyetu, muda, au pesa. Tukimpa Yeye atatulipa. |

| | C4 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Kwanza – Kifo cha Kristo<br>Mada – Busu la msaliti | C4 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Kwanza – Bwana Yesu<br>Mada – Ahukumiwa na kusulubiwa |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mathayo 26: 36-56***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 26: 39***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu aliomba katika bustani ya Gethsemane na akasalitiwa na Yuda kwa wenye mamlaka.<br>2. Umuhimu wa maombi katika nyakati ngumu. | **Neno la Biblia:** ***Luka 23: 1-33***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Warumi 5: 8***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Yesu alihukumiwa kifo japokuwa hakuwa na hatia.<br>2. Ilikuwa ni mpango wa Mungu wa wokovu kuwa Yesu asulubiwe msalabani kwa ajili ya dhambi zetu. |
| **TOA UTANGULIZI** | Waulize watoto ni aina gani ya matukio yanayowafanya wawe na wasiwasi, kufadhaika au kuogopa.<br>Wangefanya nini ili kufanya mambo kuwa rahisi kwao? | Waulize wanafunzi kama wamewahi kutuhumiwa kwa jambo ambalo hawakufanya. Waambie watengeneze orodha ya hisia walizokuwa nazo katika uzoefu huu. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Yesu na wanafunzi wake walikwenda kwenye bustani ya Gethsemane. Aliwaomba wakeshe pamoja nae. Yesu alijua yale yatakayompata, jambo ambalo lilimhuzunisha sana. ***(26: 36-38)***<br>2. Katika maombi yake, Yesu alisema kuwa alikuwa tayari kufanya chochote ambacho Baba yake alitaka afanye. Mawazo kuhusu mateso yote aliyopaswa kukumbana nayo yalimtia huzuni sana. ***(26: 39)***<br>3. Mara tatu Yesu alikuja kwa wanafunzi wake na kila wakati walikuwa wamelala. ***(26: 40-44)***<br>4. Ndipo mwanafunzi wa Yesu, Yuda, akaja na kumsaliti kwa askari. ***(26: 47-49)***<br>5. Yesu angeweza kutoroka lakini alienda kwa hiari pamoja na askari kwa sababu alijua kuwa haya yalikuwa mapenzi ya Baba. ***(26: 47-56)***<br>6. *Fikiria jinsi ilivyokuwa muhimu kwa Bwana Yesu kuwa mtiifu ili kutimiza mapenzi ya Baba yake na kwenda msalabani kwa ajili ya wokovu wa wanadamu.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Busu la msaliti. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Yesu alihukumiwa na liwali wa Kirumi Pilato. Alishtakiwa kwa kupinga malipo ya kodi kwa Kaisari na kudai kuwa yeye ni Kristo Mfalme. Pilato alitangaza kuwa hakuwa na hatia. ***(23: 1-4)***<br>2. Pilato alipotambua kuwa Yesu anatoka Galilaya, alimpeleka kwa Mfalme Herode ambaye alikuwa msimamizi wa eneo hilo. Mfalme Herode alimdhihaki na kumkejeli na kumrudisha kwa Pilato kwa sababu hakuona kosa lolote kwake. ***(23: 6-15)***<br>3. Pilato alikuwa na mfungwa mwingine aitwaye Baraba, aliyeua mtu. Wakati huu wa mwaka, kwa kawaida alimwachilia mfungwa mmoja na alitaka kumwachilia Yesu. Watu walimtaka Pilato amfungue Baraba na amsulubishe Yesu. ***(23: 18-23)***<br>4. Pilato alikuwa dhaifu sana asiweze kuonyesha msimamo mbele ya watu, hivyo akawaruhusu wamchukue Yesu ili wamsulubishe. ***(23: 24-25)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Ahukumiwa na kusulubiwa. |
| **REJELEA SOMO** | Andika taarifa saba zifuatazo kwenye vipande tofauti vya karatasi. Zichanganye na uwaambie watoto wazipange kwa mpangilio unaofaa<br>1. Yesu alikwenda Gethsemane pamoja na wanafunzi wake.<br>2. Yesu aliwachukua wanafunzi watatu akaenda nao kuomba.<br>3. Wanafunzi watatu walilala usingizi<br>4. Yuda alifika na kundi kubwa la watu<br>5. Yuda alimbusu Yesu.<br>6. Askari walimkamata Yesu.<br>7. Wanafunzi wote walikimbia. | Kesi ya Yesu mara nyingi imeelezwa kuwa ni kinyume cha sheria kabisa. Waulize wanafunzi kufikiria ni mambo mangapi yalitendeka kwa Yesu katika habari hii ambayo hayakuwa ya haki au kinyume cha sheria |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>Ni kwa namna gani Wakristo ‘humsaliti’ Bwana Yesu leo? Jadili jinsi wanavyoweza kuzuia hili lisitokee. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>Je, nimemshukuru Yesu kwa kufa msalabani kwa ajili ya dhambi zangu? (Mstari Muhimu)<br>Je, ninasimama kwa ajili ya Yesu wakati watu wengi ulimwenguni wanamchukia na kuwadhihaki walio wake? |

| | C4 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Pili – Kifo cha Kristo<br>Mada – Maamuzi ya liwali | C4 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Pili – Bwana Yesu<br>Mada – Azikwa na kufufuka! |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Mathayo 27: 1, 2, 11-31***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Mathayo 27: 22***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Pilato, liwali wa Kirumi alijua kuwa Yesu hakuwa na hatia, lakini kutokana na shinikizo, Pilato alimfungua muuaji na kumtoa Yesu asulubiwe.<br>2. Ilikuwa ni mpango wa Mungu wa wokovu kuwa Yesu asulubiwe msalabani kwa ajili ya dhambi zetu. | **Neno la Biblia:** ***Luka 23: 44-56 & 24: 1-12***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***2 Timotheo 2: 8***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Baada ya Yesu kufa, Yusufu alichukua mwili wake na kuuzika katika kaburi jipya.<br>2. Katika muda wa siku chache, kama Yesu alivyowaambia wanafunzi Wake, kaburi lilikuwa tupu, na Yesu alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu! |
| **TOA UTANGULIZI** | Waulize wanafunzi washirikishe baadhi ya chaguzi walizopaswa kufanya hivi karibuni. Waambie waorodheshe chaguzi nzuri na chaguzi mbaya. Je, waliona ni rahisi au vigumu kufanya maamuzi? | Waulize wanafunzi kushirikisha nyakati za huzuni au nyakati za giza ambazo zimewapata. Waambie walinganishe matukio hayo na matukio fulani ya furaha maishani mwao. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Baada ya kukamatwa kwake, Yesu hatimaye alipelekwa kwa Liwali wa Kirumi, Pilato. Yesu hakujibu maswali ya Pilato. Pilato alikuwa na hakika kuwa Yesu hakuwa ametenda kosa lolote. ***(27: 11-14)***<br>2. Pilato alikuwa na mfungwa mwingine aitwaye Baraba, aliyeanzisha ghasia na kuua mtu. Wakati huu wa mwaka, kwa kawaida alimfungua mmoja wa wafungwa na alitaka kumfungua Yesu. Watu walidai Pilato amfungue Baraba na kumsulubisha Yesu. ***(27: 15-23)***<br>3. Pilato aliona hapati mwelekeo wowote, na kwamba kungekuwa na ghasia kama angemfungulia Yesu. Hivyo Pilato alikubali shinikizo la umati na kuwaruhusu wamchukue Yesu akasulubiwe, kisha akamfungua Baraba. ***(27: 24-26)***<br>4. *Sisi sote lazima tuamue tutafanya nini kwa Bwana Yesu. Tunaweza ama kumpokea kama Bwana na Mwokozi wetu au kukataa kumpokea katika mioyo na maisha yetu.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Maamuzi ya liwali. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Baada ya Yesu kufa siku ya Ijumaa alasiri, mtu mmoja aitwaye Yusufu kutoka mji wa Arimathaya alipewa ruhusa ya kuushusha mwili wa Yesu msalabani na kuuweka kaburini. Akavingirisha jiwe kubwa kwenye mlango wa kaburi. ***(23: 50-53)***<br>2. Siku ya Jumapili asubuhi, baadhi ya wanawake walikuja na manukato kuupaka mwili wa Yesu. Waligundua kuwa jiwe lilikuwa limeondolewa na kuwa mwili wa Yesu haukuwepo. ***(24: 1-3)***<br>3. Malaika wawili walitokea na kuwaambia wanawake kuwa Yesu yu hai. ***(24: 4-8)***<br>4. Wanawake walikimbia kwenda kuwaambia wanafunzi. Wanafunzi walistaajabu sana wasiweze kuwaamini wale wanawake. ***(24: 9-11)***<br>5. Petro akakimbilia kaburini kutazama, lakini akaondoka akiwa anashangaa ni nini kimetokea. ***(24: 12)***<br>6. *Tumia* ***1 Wakorintho 15: 3-4*** *kuandika kwa muhtasari umuhimu wa tukio hili kuu.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Azikwa na kufufuka |
| **REJELEA SOMO** | Waambie watoto waorodheshe tofauti nyingi wawezavyo kati ya Yesu na Baraba. | Kutoka katika Usomaji wa Biblia wa funzo hili, zingatia miitikio tofauti ya a) afisa wa Kirumi, b) umati wa watu, c) wanawake Jumapili asubuhi, d) wanafunzi, na e) Petro. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>Pilato aliiruhusu kushawishiwa na shinikizo la umati. Sisi pia, tunapaswa kuwa waangalifu ili tusije tukapotoshwa na wengine ambao wanaweza kutuongoza kufanya maamuzi mabaya! | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>Soma ***Warumi 10: 9*** na ufikirie maana yake kwa kila mtu |

| | C4 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Tatu – Kifo cha Kristo<br>Mada – Kaburi la tajiri | C4 – DARAJA LA TATU<br>Funzo la Tatu – Bwana Yesu<br>Mada – Aonekana na kusikika |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Marko 15: 37, 42-47 na Marko 16: 1-8***<br><br>**Mistari Muhimu:** ***1 Wakorintho 15: 3-4***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Baada ya Yesu kufa, Yusufu alichukua mwili wake na kuuzika katika kaburi jipya.<br>2. Baada ya muda wa siku chache, kama Yesu alivyowaambia wanafunzi Wake, kaburi lilikuwa tupu, na Yesu alikuwa amefufuka kutoka kwa wafu! | **Neno la Biblia:** ***Luka 24: 13-35***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 24: 26***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Siku ile ile Yesu alipofufuka kutoka kwa wafu, aliungana na wafuasi wake wawili waliokuwa wakienda Emau.<br>2. Kama ilivyokuwa kwa watu wengi, walichanganyikiwa juu ya yote yaliyotokea na hawakuelewa kuwa Yesu alikuwa hai. |
| TOA UTANGULIZI | Waulize wanafunzi kushirikisha nyakati za huzuni au nyakati ngumu ambazo zimewapata. Waombe walinganishe matukio hayo na matukio fulani ya furaha maishani mwao. | Waulize wanafunzi wamewahi kutembea umbali gani katika safari moja. Walizungumza kuhusu nini katika safari yao? Katika habari hii wasafiri wawili walitembea kilomita kumi na moja na kurudi tena siku hiyo hiyo. Wasaidie wanafunzi kuelewa jinsi palivyokuwa mbali. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Baada ya Yesu kufa siku ya Ijumaa alasiri, mtu mmoja aitwaye Yusufu kutoka mji wa Arimathaya alipewa ruhusa ya kuushusha mwili wa Yesu msalabani na kuuweka kaburini. Akavingirisha jiwe kubwa kwenye mlango wa kaburi. ***(15: 42-47)***<br>2. Siku ya Jumapili asubuhi, baadhi ya wanawake walikuja na manukato kuupaka mwili wa Yesu. Waligundua kuwa jiwe lilikuwa limeondolewa na kuwa mwili wa Yesu haukuwapo. ***(16: 1-5)***<br>3. Malaika alitokea na kuwaambia wale wanawake kuwa Yesu yu hai. ***(16: 6)***<br>4. Malaika aliwaagiza wanawake wakawaambie wanafunzi kile kilichotokea. Wanawake waliogopa sana, kwa hiyo walikimbia na hawakumwambia mtu yeyote. ***(16: 7-8)***<br>5. *Tumia* ***1 Wakorintho 15: 3-4*** *(Mistari Muhimu) kuelezea kwa muhtasari umuhimu wa tukio hili kuu.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la tatu**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Kaburi la tajiri. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Wafuasi wawili wa Yesu walikuwa wakitembea kutoka Yerusalemu kwenda Emau. Walichanganyikiwa sana kwa yote yaliyotokea. ***(24: 13-15)***<br>2. Msafiri mwingine aliandamana nao, lakini hawakumtambua kuwa ni Yesu. Walifikiri alikuwa mgeni. Walieleza kuwa walikuwa na huzuni kwa sababu Yesu alikuwa amekufa. ***(24: 18-24)***<br>3. Walipokuwa wakitembea, Yesu alieleza jinsi Agano la Kale katika unabii mwingi lilivyotabiri matukio yote ambayo yalikuwa yametokea huko Yerusalemu. ***(24: 25-27)***<br>4. Kwa kuwa kumekuchwa na mchana unakwisha wakamshawishi wakisema, kaa pamoja nasi. Akaingia ndani kukaa nao. Walipokuwa wakila, mara wakatambua kuwa yule mgeni ni Yesu; mara Akatoweka! ***(24: 28-31)***<br>5. Wanafunzi hao wawili walirudi Yerusalemu kwa haraka sana usiku wa manane ili kuwaambia wengine yaliyotokea, na kuleta habari njema kwamba Yesu yu hai. ***(24: 33-35 )***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Aonekana na kusikika. |
| REJELEA SOMO | • Kuna ushahidi gani katika habari hii kuwa Yesu alikufa kweli?<br>• Kuna ushahidi gani katika habari hii kuwa Yesu alifufuka kweli?<br>• Je, unawezaje kumshawishi mtu ambaye hana uhakika kuhusu matukio haya kuwa yalikuwa ya kweli? | • Wasafiri wawili walijisikiaje mwanzoni mwa habari?<br>• Walijisikiaje mwishoni mwa habari?<br>• Unafikiri ni nini kilileta tofauti?<br>• Chunguza baadhi ya nabii ambazo Yesu alizitumia kuonyesha kuwa alipaswa kufa! |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>Ikiwa nimemwamini Bwana Yesu kama Mwokozi wangu, ninapaswa kuwa tayari kufanya kila njia ili kuhakikisha kuwa watu wengine wanajua kumhusu, na hasa kuwa YU HAI! | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>Ikiwa nimemwamini Bwana Yesu kama Mwokozi wangu, ninapaswa kuwa tayari kutoka nilipo ili kuhakikisha kuwa watu wengine wanamjua, na hasa ukweli kuwa YU HAI! |

| | C4 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Kifo cha Kristo<br>Mada – Maneno ya mgeni | C4 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Bwana Yesu<br>Mada – Atiliwa mashaka na kuaminiwa |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Luka 24: 13-35***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Luka 24: 26***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Siku ile ile Yesu alipofufuka kutoka kwa wafu, aliungana na wafuasi wake wawili kwenda Emau.<br>2. Kama ilivyokuwa kwa watu wengine walichanganyikiwa kuhusu yote yaliyotokea na hawakuelewa kuwa Yesu alikuwa hai. | **Neno la Biblia:** ***Yohana 20: 19-31***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Yohana 20: 29***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Baada ya kufufuka kutoka kwa wafu, Yesu aliwatokea wanafunzi wake. Tomaso hakuwepo na hakuamini kuwa wengine walikuwa wamemwona Yesu kweli.<br>2. Sijamwona Bwana Yesu aliyefufuka, lakini Yesu alisema, “Heri wale ambao hawajaona lakini wameamini”. |
| TOA UTANGULIZI | Waulize watoto ni umbali gani ambao wamewahi kutembea katika safari moja. Walizungumza nini? Katika habari hii wasafiri wawili walitembea kilomita kumi na moja, na kurudi tena siku hiyo hiyo. Wasaidie watoto kuelewa huu umbali ulivyokuwa. | Je, rafiki aliwahi kusimulia habari ya kweli ambayo uliona ni vigumu kuiamini? Waulize baadhi ya wanafunzi kutoa mifano ya habari kama hizo. Walijisikiaje walipogundua kuwa hata hivyo habari hiyo ilikuwa ya kweli? |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Wafuasi wawili wa Yesu walikuwa wakitembea kutoka Yerusalemu kwenda Emau. Walichanganyikiwa sana kwa yote yaliyotokea. ***(24: 13-15)***<br>2. Msafiri mwingine aliungana nao, lakini hawakumtambua kuwa ni Yesu. Walifikiri alikuwa mgeni. Walieleza kuwa walikuwa na huzuni kwa sababu Yesu alikuwa amekufa. ***(24: 18-24)***<br>3. Walipokuwa wakitembea, Yesu alieleza jinsi Agano la Kale katika nabii nyingi yalivyotabiriwa matukio yote ambayo yalikuwa yametokea huko Yerusalemu. ***(24: 25-27)***<br>4. Kwa sababu usiku ulikuwa unaingia, wanafunzi walimshawishi Yesu abaki nao. Walipokuwa wakila, mara wakatambua kuwa yule mgeni ni Yesu; mara Akatoweka! ***(24: 28-31)***<br>5. Wanafunzi hao wawili walirudi Yerusalemu kwa haraka sana usiku wa manane ili kuwaambia wengine yaliyotokea, na kuleta habari njema kuwa Yesu yu hai. ***(24: 33-35)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Maneno ya mgeni. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Ingawa walikuwa wamesikia kuwa Yesu amefufuka, wanafunzi walikuwa wamejifungia ndani kwa sababu waliwaogopa viongozi wa Kiyahudi. ***(20: 19)***<br>2. Usiku huohuo, Yesu alitokea ghafla ndani ya nyumba iliyofungwa. Aliwaonyesha majeraha ya kusulubiwa kwake. Hili liliwasadikisha kuwa kweli alikuwa hai na kuwafanya wajae furaha. ***(20: 20)***<br>3. Mmoja wa wanafunzi, aitwaye Tomaso, hakuwepo usiku huo na hakuamini kuwa wengine walikuwa wamemwona Yesu kweli. Alitaka kushuhudia yeye mwenyewe kabla ya kuamini. ***(20: 24-25)***<br>4. Wiki moja baadaye, wanafunzi wote, pamoja na Tomaso, walikuwa pamoja tena. Yesu akawatokea kama alivyofanya awali. Akamwonyesha Tomaso mikono na miguu Yake, hivyo Tomaso akajua kweli alikuwa ni Yesu. ***(20: 26-27)***<br>5. Basi Tomaso akajua ya kuwa Yesu yu hai, akamwita “Bwana wangu na Mungu wangu.” ***(20: 28)***<br>6. *Tomaso mara nyingi anaitwa “Tomaso mwenye shaka” kwa sababu hakuamini hadi alipomwona Yesu akiwa hai. Leo hatuwezi kumwona, lakini tunaweza kuamini kuwa yu hai na sasa yuko Mbinguni.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho B – Atiliwa mashaka na kuaminiwa. |
| REJELEA SOMO | • Wasafiri wawili walijisikiaje mwanzoni mwa habari?<br>• Walijisikiaje mwishoni mwa habari?<br>• Unafikiri ni nini kilileta tofauti?<br>• Chunguza baadhi ya unabii ambao Yesu aliutumia kuonesha kuwa alipaswa kufa. | • Ni nini kilichowashawishi wanafunzi kuwa kweli walikuwa wamemwona Yesu?<br>• Ni nini kilichomshawishi Tomaso kuwa alikuwa amekosea?<br>• Je, Mstari Muhimu unawezaje kutumika kwako leo?<br>• Angalia ***Yohana 20: 30-31*** na ufikirie kwa nini Yohana aliandika injili yake kwa jinsi alivyofanya. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>Wanafunzi walifurahi sana kutambua kuwa Yesu alikuwa hai! Alikuwa amethibitisha kuwa alikuwa kweli Mwana wa Mungu. Walitaka kuwaambia wengine habari hii njema.<br>Je, hii inaweza kuleta matokeo gani katika maisha yetu leo? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>Baadhi ya watu leo wanaweza kutilia mashaka kuwa Yesu yu hai kwa sababu hawajamwona. ***Yohana 20: 29*** inawahakikishiaje wale wanaoamini? |

| | C5 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Kwanza – Ruthu<br>Mada – Maamuzi mabaya | C5 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Kwanza – Ruthu<br>Mada – Familia kuwa mbali na Mungu |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Ruthu 1: 1-14***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Waamuzi 21: 25***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Habari katika Ruthu Sura ya 1 inahusisha watu mbalimbali wanaofanya maamuzi.<br>2. Nyakati zingine, sote tunapaswa kufanya maamuzi muhimu. Tunapaswa kumshirikisha Mungu tunapoyafanya. Maamuzi yetu yanaweza kuathiri wengine. | **Neno la Biblia:** ***Ruthu 1: 1-14***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Waamuzi 21: 25***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Habari katika Ruthu Sura ya 1 inahusisha watu mbalimbali wanaofanya maamuzi.<br>2. Maamuzi yetu yana matokeo mazuri au mabaya; ni vyema kuomba msaada wa Mungu katika kuyafanya. |
| **TOA UTANGULIZI** | Katika vikundi au wawiliwawili waambie watoto wajadili:<br>• Sababu zinazofanya watu kuhama na kwenda kuishi katika eneo au nchi ya ugenini.<br>• Matatizo wanayoweza kukabiliana nayo wanapokwenda kuishi katika mazingira mapya.<br>Mawazo yanaweza kuorodheshwa au kuonyeshwa kama michoro ya 'buibui'. Vinginevyo, ikiwa watoto wamehamia eneo jipya, wanaweza kuwa tayari kushirikisha uzoefu wao. | Maamuzi ni muhimu kiasi gani? Onyesha mifano ya maamuzi na waambie wanafunzi wakadirie umuhimu wake kwa kushikilia moja ya kadi tatu - X (sio muhimu), ~ (muhimu kiasi) ! (muhimu sana)<br>Mifano: Chakula gani cha kula mchana, kulala kitandani au kwenda kanisani, ni rangi gani za nguo za kununua, kama ni muhimu kumwamini Yesu kama Mwokozi wako, ni masomo gani ya kujifunza, kuripoti tukio la uonevu, n.k. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Israeli walikuwa wamemwacha Mungu; kila mtu alifanya yaliyokuwa ni mema machoni pake mwenyewe. ***(Mstari muhimu)***<br>2. Hahari hii inapoanza, watu wanafanya maamuzi muhimu, baadhi yao ni mazuri kuliko mengine. Elimeleki, Naomi, na wana wao, Maloni na Kilioni waliishi Bethlehemu, ambayo maana yake ni 'Nyumba ya Mkate', lakini kulikuwa na njaa katika nchi. Elimeleki aliamua kuipeleka familia yake Moabu, nchi ambayo watu waliabudu sanamu. Hatujaambiwa kuwa aliomba. *Je, alipaswa kumwamini Mungu kuwatoa katika nchi yao wenyewe?* ***(1: 1-2)***<br>3. Huko Moabu msiba ulitokea; Elimeleki alikufa. Maloni na Kilioni wakaoa wasichana wa Moabu, Ruthu & Orpa, lakini Maloni na Kilioni pia walikufa. ***(1: 3-5)***<br>4. Naomi aliposikia njaa imekwisha, alitaka kurudi Bethlehemu. Wakweze wakataka kwenda naye. Alithamini wema wao lakini aliwasihi warudi kwenye familia zao. Hatimaye Orpa anarudi lakini Ruthu anaamua kuwenda na Naomi. ***(1: 6-14)***<br>5. *Elezea kwa nini Naomi alitaka wakweze warudi, na kwa nini hatimaye Orpa aliamua kurudi Moabu. Fikiria jinsi ambavyo ilikuwa vigumu kwa Ruthu kuamua kwenda nchi ya ugenini.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Maamuzi mabaya | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Muktadha: Wakati wa Waamuzi, kulikuwa na ukosefu wa viongozi wacha Mungu, kila mtu alijifurahisha mwenyewe. ***(Mstari muhimu)***<br>2. Hiyo ndiyo ilikuwa sababu ya njaa katika Israeli, licha ya ahadi ya Mungu ya nchi "itiririkayo maziwa na asali." ***(Kumbukumbu la Torati 30: 15-20)***<br>3. Elimeleki alichagua kuipeleka familia yake Moabu, nchi ya kuabudu sanamu. Mungu anapuuzwa katika mpango wao. ***(1: 1-2)***<br>4. Msiba ulitokea mara mbili; Elimeleki akafa, akamwacha Naomi mjane. Baada ya kuoa wanawake wa Moabu, Ruth & Orpa, wana Maloni na Kilion pia walikufa kabla ya wote kupata watoto. ***(1: 3-5)***<br>5. Naomi aliamua kurudi kwa sababu sasa kulikuwa na chakula huko Bethlehemu. Aliwajibika kwa wakweze. Alithamini wema wao kwake lakini alitambua kuwa hawezi kuwapa waume wapya. Naomi akawasihi warudi kwenye familia zao.<br>6. Kila mtu alifanya uchaguzi wake binafsi: Orpa alirudi, Ruthu akaenda na Naomi. ***(1: 6-18)***<br>7. *Eleza kwa nini Naomi alitaka wakweze warudi, na kwa nini hatimaye Orpa aliamua kurudi Moabu. Fikiria jinsi ambavyo ilikuwa vigumu kwa Ruthu kuamua kwenda katika nchi ya ugenini.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Familia kuwa mbali na Mungu |
| **REJELEA SOMO** | Waambie watoto waandike baadhi ya chaguzi watakazopaswa kufanya, baadhi wiki ijayo, zingine baadaye maishani. Tumia namba kuziweka katika mpangilio wa kipaumbele (1= muhimu zaidi, n.k.) | Mkiwa wawili-wawili, hebu wazia jinsi mazungumzo kati ya Ruthu na Orpa yalivyoendelea walipozungumzia faida na hasara za kwenda Bethlehemu pamoja na Naomi au kurudi kwao katika familia zao huko Moabu. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Jadili jinsi chaguzi tunazofanya zinavyokuwa na matokeo - kwetu sisi na kwa wengine. Uamuzi wa Elimeleki ulileta familia yake kwenye utamaduni ambapo Mungu hakutambuliwa. Uamuzi wa Naomi wa kurudi ulimaanisha kuwa Ruthu na Orpa nao walikuwa na maamuzi ya kufanya.<br>2. Tunaweza kupata msaada kutoka kwa Mungu tunapofanya maamuzi. (Omba, soma Biblia, omba ushauri kwa Wakristo wenye umri mkubwa zaidi).<br>3. Uamuzi wetu muhimu zaidi maishani utakuwa jinsi tunavyoitikia kwa Bwana Yesu Kristo. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Chaguzi tunazofanya zina matokeo mazuri au mabaya - kwetu sisi wenyewe na kwa wengine. Fikiria juu ya maamuzi juu ya kazi, chaguo la marafiki, ndoa, matumizi ya muda na pesa, nk.<br>2. Soma ***Mithali 3: 5 & 6 na 14: 12***. Maamuzi bora zaidi yatafanywa tunapomhusisha Mungu katika kuyafanya. Tunawezaje kufanya hivi? |

| | C5 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Pili – Ruthu<br>Mada – Kurudi kwa wajane | C5 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Pili – Ruthu<br>Mada – Naomi amrudia Mungu |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Ruthu 1: 14-22 na 2: 1-3***<br><br>**Mistari Muhimu:** ***Ruthu 1: 16-17***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Upendo wa Naomi na imani katika Mungu wa Naomi vilimsaidia Ruthu kuwa na ujasiri wa kwenda kuishi nchi ya ugenini.<br>2. Kila mmoja wetu anapaswa kuamua ikiwa ataweka tumaini lake kwa Mungu au kuwa na vipaumbele vingine katika maisha yetu. | **Neno la Biblia:** ***Ruthu 1: 15-22***<br><br>**Mistari Muhimu:** ***Ruthu 1: 16-17***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Upendo wa Naomi na imani katika Mungu wa Naomi vilimsaidia Ruthu kuwa na ujasiri wa kwenda kuishi katika nchi ya ugenini.<br>2. Imani katika Mungu na kujitoa kwake, hutuwezesha kufanya maamuzi magumu, kuchukua hatua ya kufanya tusiyoyajua.<br>3. Uaminifu kwa familia na marafiki na ibada kwa Bwana Yesu kunampendeza Mungu. |
| **TOA UTANGULIZI** | Waambie watoto wamfikirie mtu mzima ambaye wanamkubali sana. Waambie waorodheshe sababu tano kwa nini wanamkubali mtu huyo sana. Baadhi ya sababu zinaweza kushirikishwa katika kundi zima.<br>Katika habari hiyo, Ruthu amejitoa kwa mama mkwe wake. Je, sifa alizoona kwa Naomi zilimtia moyo amtumaini Mungu wa Naomi? | Waambie wanafunzi wachore mzunguko wa mkono wao kwenye karatasi. Andika 'UAMINIFU' kwenye kiganja. Kwenye kila kidole na kidole gumba andika neno au maneno ya kuonyesha maana ya kuwa mwaminifu kwa mtu fulani. Shirikisha mawazo. Ruthu alionyesha uaminifu mkubwa sana kwa Naomi, na pia kwa Mungu wa Naomi, Ruthu na Orpa walipaswa kufanya maamuzi yao wenyewe. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Ruthu na Naomi wako njiani kurudi Bethlehemu. Kisha Ruthu akaonyesha upendo wake kwa Naomi, kujitolea kwake kwa watu wa Naomi na imani yake katika Mungu wa Naomi. Kifo pekee ndicho kingewatenganisha. ***(Angalia Mstari Muhimu)***<br>2. Kulikuwa na msisimko huko Bethlehemu Naomi na Ruthu waliporudi, wakati mavuno ya shayiri yalipokuwa yanaanza. ***(1: 19)***<br>3. Majina mara nyingi huwa na maana; wakati mwingine jina linamfaa mtu, wakati mwingine sivyo. Naomi ina maana ya 'kupendeza' lakini sasa alitaka kuitwa Mara, maana yake 'uchungu'.<br>4. Naomi alikuwa na sababu za kutaka jina lake libadilishwe; alikuwa ameondoka akiwa 'amejaa', pamoja na mume wake na wanawe, lakini akarudi akiwa 'tupu', bila wao. Mwenyezi Mungu alikuwa amemletea matatizo na huzuni maishani mwake. ***(1: 20-21)***<br>5. Utayari wa Ruthu kufanya kazi ili kujitafutia riziki yeye na Naomi. Alipata kazi katika shamba la Boazi, mkulima tajiri ambaye, kwa kweli, alikuwa wa jamaa ya Elimeleki. ***(2: 1-3)***<br>6. *Fikiria jinsi Mungu alivyokuwa akifanya kazi katika maisha ya Ruthu akamleta Bethlehemu na kumpeleka kwenye shamba ambako angekutana na Boazi.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Kurudi kwa wajane. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Kulikuwa na kuagana kwa machozi huku Orpa akiamua kurudi kwa familia yake na kwenye miungu yao ya uwongo. ***(1: 14)***<br>2. Ruthu alitangaza azimio la imani yake kwa Mungu, uaminifu wake kwa Naomi, uamuzi wake wa kuishi naye, kuwakubali watu wa Naomi kuwa wa kwake, kumwamini Mungu wa Naomi kama Mungu wake, kufa ambapo Naomi atakufa. Kifo pekee ndicho kingewatenganisha. ***(Mistari muhimu)***<br>3. *Ni muhimu kuwa mwaminifu kwa familia na marafiki; kujitolea kwa Bwana Yesu ni muhimu zaidi.*<br>4. Kuwasili kwa Naomi na Ruthu huko Bethlehemu kulizua taharuki. Ilikuwa mwanzo wa mavuno ya shayiri. Naomi aliomba aitwe Mara ikimaanisha 'uchungu', badala ya Naomi ambayo ilimaanisha 'kupendeza'. Alikuwa ameondoka Bethlehemu 'amejaa', akiwa na mume na wanawe, lakini akarudi akiwa 'tupu'. ***(1: 19-22)***<br>5. *Hali zenye uchungu zilitumiwa kumrudisha Naomi katika njia yake ya kumrudia Mungu. Alikubali makosa ya zamani na Mungu, kwa fadhili zake, akamleta nyumbani salama.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Naomi amrudia Mungu. |
| **REJELEA SOMO** | Mkiwa wawili wawili, fanyeni mahojiano ya kejeli na Naomi, kila mmoja akifikiria maswali mawili au matatu ya kumuuliza. | Andika makala fupi ya gazeti la Habari za Bethlehemu, ukiipa kichwa 'Mjane Aliyekata tamaa Arudi Nyumbani'. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Ugumu wa maisha hauji kwa sababu ya maamuzi mabaya ambayo tumefanya, lakini, ikiwa tutafanya maamuzi mabaya, tunapaswa kuwa tayari kukubali kushindwa na kuomba msamaha kutoka kwa Mungu (na labda kwa wengine ambao tumewakosea) .<br>2. Je, kweli tunamwamini Mungu atusaidie tunapolazimika kukabiliana na hali mpya k.m. kubadilisha shule? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Unafikiri kwa nini Naomi alichochea uaminifu huo kwa Ruthu? Je, wengine wangependa kuweka tumaini lao kwa Kristo kwa sababu ya kile wanachokiona kwako na kwangu?<br>2. Soma ***Luka 15: 11-24 au 1 Yohana 1: 9***. Je, mistari hii inatuhamasishaje kukiri tumekosea wakati tunapokuwa tumefanya makosa (tumefanya dhambi)?<br>3. Inafundisha nini kuhusu Msamaha wa Mungu? |

| | **C5 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Tatu – Ruthu**<br>**Mada – Familia tajiri** | **C5 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Tatu – Ruthu**<br>**Mada – Wajane waongozwa na Mungu** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Ruthu 2: 1-23***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Ruthu 2: 20***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu alikuwa akiwatunza Ruthu na Naomi kwa kumleta Ruthu kwenye shamba la Boazi, jamaa yake, ambaye angemtendea mema na kumlinda dhidi ya madhara.<br>2. Hata wakati maisha ni magumu, tunaweza kumwamini Mungu kuongoza maisha yetu kwa ubora zaidi. | **Neno la Biblia:** ***Ruthu 2: 1-23***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Ruthu 2: 20***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Wakati wa mavuno ulimpa Ruthu nafasi nzuri ya kuajiriwa ili kumsaidia Naomi na yeye mwenyewe.<br>2. Boazi ni mkarimu katika kutoa matunzo na msaada wake kwa Ruthu, mgeni, akitambua kazi yake ngumu na uaminifu. Daima tunapaswa kufanya kazi kwa kiwango kinachompendeza Mungu. |
| **TOA UTANGULIZI** | Fikiria uko njiani kuelekea siku yako ya kwanza katika kazi mpya katika nchi ya ugenini. Jadili katika vikundi au wawiliwawili nini ambacho kingekuwa kikipita akilini mwako. Je mambo gani matatu yangekupa wasiwasi? | Jadili katika vikundi: Je, kazi ni nzuri kwetu, au ni 'uovu wa lazima' tu?<br>**AU**<br>Mkiwa wawiliwawili, mwajiri na mwajiriwa, jadilini viwango ambavyo kila mmoja angetarajia kuviona kwa mwenzake. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Ruthu alijitolea kufanya kazi ili kumsaidia Naomi na yeye mwenyewe. Alikwenda kwenye shamba la Boazi. Wavunaji walikata nafaka na vijakazi wakafuata nyuma ili kufunga mabua ya nafaka kuwa miganda. Mabua yoyote ambayo yalisahauliwa na vijakazi yalipaswa kuachwa kwa ajili ya maskini, wajane n.k. wayakusanye. (au kuokota masazo) ***(2: 1-3)***<br>2. Boazi, mwenye shamba, alimwona Ruthu, akauliza yeye ni nani na akapewa ripoti na msimamizi kuhusu bidii yake ya kazi. ***(2: 5-7)***<br>3. Boazi alionyesha wema kwa Ruthu. Akamwambia akae na vijakazi wake, anywe maji akiwa na kiu. Aliwaambia vijana wake wasimguse na akampa mkate na nafaka iliyookwa wakati wa chakula. ***(2: 8-9)***<br>4. Ruthu alishukuru kupita kiasi kwa wema, ambao, kama mgeni, alihisi kuwa hakustahili – *Mfano wa upendo na neema ya Mungu (neema yake tusiyostahili) kwetu.* ***(2: 10-13)***<br>5. Boazi alivutiwa na uaminifu wa Ruthu kwa Naomi na kwa Mungu ambaye alikuwa amemtumaini<br>6. Naomi alifurahishwa na siku ya mafanikio ya Ruthu na habari za Boazi. ***(2: 17-23)***<br>7. *Mungu alikuwa na mpango na alikuwa akiongoza maisha yao.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu**.<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Familia tajiri | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Sheria ya Mungu ilisema kuwa nafaka iliyoachwa na wavunaji bila kukatwa kando kando ya shamba, na mabua yoyote yaliyoangushwa na vijakazi walipofunga miganda yangeachwa kwa wajane na maskini, kama Ruthu, ili wachukue (hii inaitwa kuokota masazo). ***(2: 1-3)***<br>2. 'Ikatokea' Ruthu (Huu ulikuwa ni mwongozo wa Mungu!) kufanya kazi katika shamba la Boazi, jamaa ya Elimeleki. Alimwona na kuuliza juu ya Ruthu na akaambiwa na msimamizi kuhusu bidii yake ya kazi. ***(2: 5-7)***<br>3. Boazi alionyesha wema kwa Ruthu. Alimwambia akae na vijakazi wake, anywe maji akiwa na kiu, akawaambia vijana wake wasimguse na akampa mkate na nafaka iliyookwa wakati wa chakula. ***(2: 8-9)***<br>4. Ruthu alishukuru kupita kiasi kwa wema, ambao, kama mgeni, alihisi kuwa hakustahili – *Huu ni mfano wa upendo na neema ya Mungu (neema yake tusiyostahili) kwetu.* ***(2: 10-13)***<br>5. Boazi, kama mtu wa Mungu, alistaajabu bidii ya kazi ya Ruthu, uaminifu wake kwa Naomi na kwa Mungu 'ambaye alikimbilia chini ya mbawa zake'. ***(2: 11-12)***<br>6. Naomi alifurahi kusikia habari za Boazi. ***(Mstari muhimu)***<br>7. *Ruthu alijikuta akiokota masazo katika shamba la Boazi, jamaa ya Elimeleki. Katika hili, na wakati wa kuwasili kwao, tunaona kuwa Mungu alikuwa akiwatendea mema.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Wajane waongozwa na Mungu. |
| **REJELEA SOMO** | Mkifanya kazi wawiliwawili, tengenezeni maswali matano ya jaribio kulingana na somo la leo. Vikundi viwili vinaweza kupimana kwa maswali yao ya jaribio. | Siku yangu ya kwanza kazini Bethlehemu'. Jione kama wewe ni Ruthu unayeandika maelezo mwisho wa siku. Je, angeandika mawazo au maoni gani? |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Kumwamini Mungu hakukumfanya Ruthu kuwa mvivu. Je, unaweza kutarajia Mungu akusaidie katika mitihani ikiwa hujafanya kazi kwa bidii katika kufanya marudio?<br>2. Mwanafunzi mgeni anajiunga na darasa lako. Je, ungemsaidia na kufanya urafiki naye kama Boazi alivyofanya kwa Ruthu au ungebaki tu na marafiki zako na kumpuuza? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>Kwa siku moja, Ruthu alikusanya karibu kilo 10 za shayiri - ambayo ilikuwa ni kazi kubwa ya kurudia-rudia, ya kuchosha mgongo!<br>Soma ***Wakolosai 3: 22-24***.<br>Kwa jinsi gani mfano wa Ruthu na mistari hii inashawishi mtazamo wetu wa kufanya kazi? |

| | C5 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Ruthu<br>Mada – Mapenzi ya Mungu | C5 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Ruthu<br>Mada – Boazi na Ruthu wabarikiwa na Mungu |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***Ruthu 3: 1-18 & 4: 1-17***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Zaburi 37: 5***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Naomi alitaka Ruthu awe na maisha salama baadae hivyo alisaidia kupanga ndoa na pia kurudisha ardhi ya Elimeleki kwa Ruthu.<br>2. Mungu akawabariki Ruthu na Naomi. Baada ya kuchagua kumfuata Mungu badala ya sanamu, Ruthu akawa sehemu ya mpango wa Mungu kwa ajili ya wokovu wetu. | **Neno la Biblia:** ***Ruthu 3: 1-18 & 4: 1-17***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***Ruthu 4: 10***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Naomi alitaka kuhakikisha usalama wa maisha ya Ruthu ya baadaye. Alimwona Boazi wa jamaa yao kuwa 'mkombozi wa jamaa ya karibu' ambaye angenunua shamba lao na kumwoa Ruthu ili shamba hilo libakie kwenye familia.<br>2. Ruthu na Naomi wanabarikiwa kupita matarajio. Baada ya kuchagua kumfuata Mungu badala ya sanamu, Ruthu akawa sehemu ya mpango wa Mungu wa wokovu. |
| TOA UTANGULIZI | Waambie wanafunzi waunde 'mti wa familia' kwenye karatasi. Angalia ikiwa kuna yeyote anayeweza kufuatilia vizazi hadi babu wa babu zao. | Kuna baadhi ya tamaduni ambapo wazazi wanahusika katika kupanga ndoa kwa watoto wao. Mkiwa wawiliwawili, jadilini faida na hasara za kufanya hivi. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Mpango wa Naomi ulikuwa Ruthu kumwendea Boazi, kumwomba awe mkombozi wao wa jamaa ya karibu, yaani, kununua tena shamba la Elimeleki na kumwoa Ruthu. ***(3: 1-2)***<br>2. Ilikuwa jioni wakati wa mavuno. Baada ya kula na kunywa, Boazi angelala kando ya lundo la nafaka ili kulilinda dhidi ya wezi.<br>3. Naomi alimwambia Ruthu avae mavazi yake mazuri, aende kwa Boazi, aliyekuwa amelala kando ya nafaka. Ruthu alikuwa mtiifu, akaenda kwa Boazi, akalala na kusubiri. ***(3: 3-7)***<br>4. Boazi aliamka ghafla wakati wa usiku na kumkuta Ruthu miguuni pake. Alimwomba amfunike kwa pembe ya vazi lake kama ishara kuwa, angefanya kama mkombozi wa jamaa yao. ***(3: 8-9)***<br>5. Aliahidi kusaidia, lakini kulikuwa na jamaa wa karibu ambaye lazima kwanza aulizwe. Boazi alimrudisha Ruthu nyumbani alfajiri na kumpa Naomi nafaka. ***(3: 10-15)***<br>6. Kesho yake asubuhi Boazi akakutana na wazee kumi na yule jamaa mwingine kwenye lango la mji. Kwa kuwa mwanamume huyo hakutaka kumwoa Ruthu, Boazi alikubali kufanya hivyo na kumnunulia shamba hilo. ***(4: 1-6)***<br>7. Naomi alifurahi sana walipopata mtoto, aliyeitwa Obedi, ambaye mjukuu wake angekuwa Mfalme Daudi. ***(4: 16-17)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Mapenzi ya Mungu. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Naomi alikuwa na wasiwasi kwa ajili ya maisha yao ya baadaye – hitaji la 'mkombozi wa jamaa ya karibu' kununua ardhi yao na kumwoa Ruthu, hivyo kuirudisha ardhi ndani ya familia. Alipendekeza kuwa Ruthu amuendee Boazi faraghani kwa ajili ya ombi hilo mwisho wa siku jioni. ***(3: 1-2)***<br>2. Baada ya kupura nafaka, wanaume walikula, kunywa na kulala kando ya lundo la nafaka ili kuwazuia wezi.<br>3. Ruthu alioga, akatia manukato, na kuvaa mavazi yake bora, kama bibi-arusi anavyovaa, akaenda kwa Boazi akiwa amelala kando ya nafaka. Kufunua miguu yake kama alivyoelekezwa na Naomi naye akajilaza akisubiri. ***(3: 3-6)***<br>4. Kwa kushtushwa na jambo fulani, Boazi aliamka na kumkuta Ruthu akiwa amelala miguuni pake. Alimwomba amfunike kwa pembe ya vazi lake kama ishara kuwa, angekuwa mkombozi wa jamaa yao. ***(3: 9)***<br>5. Boazi alikuwa na hamu ya kusaidia lakini jamaa wa karibu lazima aombwe kwanza. Ruthu alirudishwa nyumbani alfajiri pamoja na nafaka kwa Naomi. ***(3: 10-15)***<br>6. Kesho yake asubuhi, Boazi akakutana katika lango la mji na wazee kumi na yule jamaa mwingine wa ukoo. Kwa vile mtu huyu hakutaka kumwoa Ruthu, Boazi alisema angemwoa; mjadala ulihitimishwa kwa kuvuliwa kiatu. ***(4: 1-8)***<br>7. Naomi alifurahi sana walipopata mtoto, aliyeitwa Obedi, ambaye mjukuu wake angekuwa Mfalme Daudi. ***(4: 16-17)***<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Boazi na Ruthu wabarikiwa na Mungu. |
| REJELEA SOMO | Tengeneza alama, ukiandika juu yake sehemu fulani ya **Mstari Muhimu**. Unapofanya kazi, fikiria jinsi habari ya Ruthu inavyofafanua mstari huu. | Mkiwa wawiliwawili au vikundi vidogo, tayarisheni mahojiano ya Televisheni na Boazi na Ruthu baada ya ndoa yao. Wasichana wangependa kumuuliza nini Ruthu, na wavulana wangependa kumuuliza nini Boazi? |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>• Miaka 1000 baadaye, pia huko Bethlehemu, Mungu aliruhusu Mwanawe azaliwe katika familia iliyotokana na Boazi na Ruthu. Kwa hivyo, msichana kutoka Moabu, ambaye aliwahi kuabudu sanamu, anakuwa sehemu ya habari ya mpango wa Mungu wa wokovu wetu -<br>• Uamuzi wake wa kumwamini Mungu ulikuwa wa muhimu kiasi gani?<br>• Tunapomwamini Mungu, na Bwana Yesu kama Mwokozi wetu nani ajuaye matokeo ya uamuzi huo yanaweza kuwa nini? Mungu pekee ndiye anajua! | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>Soma ***1 Wakorintho 6: 19-20 & 1 Petro 1: 18-19***.<br>• Kristo alilipa gharama gani ili kutukomboa sisi tuliokuwa wenye dhambi, na kuturudisha katika familia ya Mungu?<br>• Ikiwa tumenunuliwa kwa gharama ya ajabu sana, tunapaswa kumheshimu (kumletea utukufu) Mungu, badala ya kujifurahisha wenyewe<br>• Je, tunafanyaje hili katika mitazamo yetu na chaguzi tunazofanya siku baada ya siku? |

| | C6 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Kwanza – Samweli<br>Mada – Kumwomba Mungu | C6 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Kwanza – Samweli<br>Mada – Kumwomba Mungu |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***1 Samweli 1: 1-28***<br><br>**Mistari Muhimu:** ***1 Samweli 1: 10-11***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Hana alimwomba Mungu kwa ajili ya mtoto.<br>2. Mungu anaweza kusikia na kujibu maombi yetu wakati wa mahitaji. | **Neno la Biblia:** ***1 Samweli 1: 1-28***<br><br>**Mistari Muhimu:** ***Mathayo 6: 5-8***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Hana alimwomba Mungu kwa ajili ya mtoto<br>2. Mungu husikia na kujibu maombi yetu. |
| TOA UTANGULIZI | Orodhesha mambo 5 makuu ambayo unafikiri watu wanayaomba. Kisha jadili mawazo yako na kikundi. | Jadili yafuatayo kwanza mkiwa wawiliwawili, kisha ungana na wengine kusikiliza mawazo yao<br>1. Kwa nini watu huomba?<br>2. Kuna haja ya kuzingatia jinsi unavyoomba?<br>3. Watu wengi huomba nini?<br>4. Watu huomba wakati gani? |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Elkana alikuwa na wake wawili - Penina na Hana. Penina alikuwa na watoto lakini Hana hakuwa na watoto. ***(1: 1-2)***<br>2. Walipotembelea Nyumba ya Bwana, Hana alihuzunika sana kwa sababu Penina alimtesa. Alilia na kumwomba Mungu. ***(1: 3-10)***<br>3. Hana alimwahidi Mungu kuwa kama angempa mtoto wa kiume, angemtoa kwa Mungu. ***(1: 11)***<br>4. Kuhani Eli alimdhihaki Hana akidhani kuwa amelewa, kwa sababu midomo yake ilionekana kama anena lakini sauti yake haikusikika.<br>5. Hana alieleza kwamba alikuwa akimimina moyo wake kwa Mungu. Eli alitambua kuwa alikuwa akizungumza ukweli na akambariki. ***(1: 12-18)***<br>6. Mungu akamkumbuka Hana, akampa mtoto wa kiume. Hana akamwita Samweli na akatimiza ahadi yake, akamtoa kwa Bwana. ***(1: 20)***<br>7. *Elezea kuwa tunaweza kuleta matatizo yetu yote kwa Mungu katika sala, lakini sikuzote Yeye hajibu jinsi tunavyoweza kutazamia.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Kumwomba Mungu. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Elkana alikuwa na wake wawili - Penina na Hana. Penina alikuwa na watoto lakini Hana hakuwa na watoto ***(1: 1-2)***<br>2. Walipotembelea Nyumba ya Bwana, Hana alihuzunika sana kwa sababu Penina alimtesa. Alilia na kumwomba Mungu. ***(1: 3-10)***<br>3. Hana alimwahidi Mungu kwamba kama angempa mtoto wa kiume, angemtoa kwa Mungu. ***(1: 11)***<br>4. Kuhani Eli, alimhukumu Hana vibaya na akafikiri kuwa alikuwa amelewa, kwa sababu midomo yake ilikuwa ikinena lakini hakuwa akisema chochote<br>5. Hana alieleza kuwa alikuwa akimimina moyo wake kwa Mungu. Eli alitambua kuwa alikuwa akizungumza ukweli na akambariki. ***(1: 12-18)***<br>6. Mungu akamkumbuka Hana, akampa mtoto wa kiume. Hana akamwita Samweli na akatimiza ahadi yake, akamtoa kwa Bwana. ***(1: 20-28)***<br>7. *Eleza kuwa tunaweza kuleta matatizo yetu yote kwa Mungu katika sala, lakini sikuzote Yeye hajibu jinsi tunavyoweza kutazamia.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Kwanza.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Kumwomba Mungu |
| REJELEA SOMO | Unda kipande cha katuni cha habari hii, ukitumia angalau picha 6 zilizo na maelezo mafupi. Tumia viputo vya hotuba inapofaa. Hii inaweza kufanywa na wawiliwawili au kikundi kidogo. | Mkiwa wawiliwawili, tengenezeni karatasi ya maelezo inayoonyesha kile ambacho umejifunza kuhusu maombi kutoka katika somo hili. Jaribu kufikiria angalau dondoo 10 na uzionyeshe kwa uangalifu. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Hana alimgeukia Mungu alipokuwa amekasirika na kufadhaika. Je, tunaweza kufanya vivyo hivyo? Sala ni muhimu kiasi gani kwa kila mmoja wetu?<br>2. Hana alitimiza ahadi yake ya kumtoa mwanawe kwa Bwana - je, sisi tunatimiza ahadi zetu kila wakati? Je, tunapaswa kuweka ahadi kwa Bwana? | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Ulitoa ahadi mara ya mwisho lini?<br>2. Je, uliitimiza?<br>3. Je, tunapaswa kuweka ahadi kwa Bwana?<br>4. Kutokana na **Mistari Muhimu** katika ***Mathayo 6: 5-8***, ni kanuni gani tunaweza kujifunza kuhusu maombi?<br>5. Fikiria wakati ambapo Mungu alijibu maombi yako na kuyashirikisha kwenye kikundi. |

| | **C6 – DARAJA LA TATU**<br>**Somo la Pili – Samweli**<br>**Mada – Kukua mbele za Mungu** | **C6 – DARAJA LA NNE**<br>**Funzo la Pili – Samweli**<br>**Mada – Kukua mbele za Mungu** |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***1 Samweli 2: 1-2, 18-21, 26, 34***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Samweli 2: 30***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Hana alibarikiwa na Mungu na akashukuru kwa kuzaliwa kwa Samweli. Kwa hiari alimtoa Samweli kwa Bwana. Samweli akazidi kukua na kupata kibali kwa Mungu.<br>2. Mungu huwaheshimu wale wanaomheshimu. | **Neno la Biblia:** ***1 Samweli 2: 1-36***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Samweli 2: 30***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Hana alibarikiwa na Mungu na akashukuru kwa kuzaliwa kwa Samweli.<br>2. Kwa hiari yake alimtoa Samweli kwa Bwana. Samweli akazidi kukua na kupata kibali kwa Mungu.<br>3. Mungu huwaheshimu wale wanaomheshimu. |
| **TOA UTANGULIZI** | Ni lini mara yako ya mwisho kumsifu Mungu? Fikiria mambo mbalimbali tunayoweza kufanya ili kumsifu Mungu, na njia mbalimbali tunazoweza kutumia katika kumsifu na kumheshimu. | Fikiria mambo mbalimbali tunayoweza kufanya ili kumsifu Mungu, na njia mbalimbali tunazoweza kutumia katika kumsifu na kumheshimu. |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Hana alifurahi kuwa Mungu alikuwa amempa mtoto wa kiume. Alimshukuru Mungu kwa jinsi alivyo na kwa yote aliyomtendea. ***(2: 1-10)*** Alifurahi kuwa alikuwa ametimiza ahadi yake na kumtoa Samweli kwa Bwana.<br>2. Samweli alilelewa akimtumikia Mungu katika Nyumba ya Mungu. Kila mwaka, mama yake alimtembelea na kumletea nguo mpya. ***(2: 18-19)***<br>3. Eli alimwomba Mungu ampe Hana watoto zaidi. Mungu alimbariki Hana na kumpa watoto wengine watano. ***(2: 20-21)***<br>4. Samweli alifanya kazi kwa bidii na kupata kibali kwa Bwana. ***(2: 26)***<br>5. Wana wa Eli walifanya dhambi na kuadhibiwa na Mungu. ***(2: 34)***<br>6. *Fikiria tofauti kati ya Samweli aliyempendeza Mungu na wana wa Eli, ambao hawakutii amri za Mungu na kuadhibiwa.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Kukua mbele ya Mungu. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Hana alifurahi kuwa Mungu alikuwa amempa mtoto wa kiume. Alimshukuru Mungu kwa jinsi alivyo na kwa yote aliyomtendea. ***(2: 1-10)*** Alifurahi kuwa alikuwa ametimiza ahadi yake na kumtoa Samweli kwa Bwana.<br>2. Samweli alilelewa akimtumikia Mungu katika Nyumba ya Mungu. Kila mwaka, mama yake alimtembelea na kumletea nguo mpya. ***(2: 18-19)***<br>3. Eli alimwomba Mungu ampe Hana watoto zaidi. Mungu alimbariki Hana na kumpa watoto wengine watano. ***(2: 20-21)***<br>4. Samweli alifanya kazi kwa bidii na kupata kibali kwa Bwana. ***(2: 26)***<br>5. Wana wa Eli walifanya dhambi na kuadhibiwa na Mungu. Waliasi amri ambazo Mungu alikuwa amewapa kuhusu majukumu yao ya kikuhani. ***(2: 34)***<br>6. *Fikiria tofauti kati ya Samweli aliyempendeza Mungu na wana wa Eli, ambao hawakutii amri za Mungu na kuadhibiwa.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Pili.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Kukua mbele ya Mungu. |
| **REJELEA SOMO** | 1. Fikiria maamuzi ambayo utalazimika kufanya katika siku zijazo. Unawezaje kumheshimu Mungu kupitia maamuzi hayo? Jadilini mkiwa wawiliwawili na kisha na kundi zima.<br>2. Tengeneza gramu ya buibui inayoonyesha njia ambazo Mungu anaweza kuheshimiwa katika maisha yako. | 1. Soma ***Zaburi 103: 1-5***. Andika maombi, ukimsifu Mungu kwa mambo mema ambayo ametenda katika maisha yako<br>2. Chunguza maisha ya Eric Liddel. Je, ni kwa jinsi gani alimheshimu Mungu?<br>3. Jadili jinsi tunavyoweza kumheshimu Mungu katika kila kazi anayotupa. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Angalia ***Wakolosai 3: 23*** tena. Tunapaswa kuwa na mtazamo gani katika kazi yetu?<br>2. Je, unamheshimu Mungu katika kila jambo unalofanya?<br>3. Omba ili Mungu akusaidie kumheshimu katika maamuzi yako. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Omba ili Mungu akusaidie kumheshimu katika maisha yako ya kila siku.<br>2. Jadili mtazamo ambao Mkristo anapaswa kuwa nao kwenye kazi yake. Soma tena ***Wakolosai 3: 23***. |

| | C6 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Tatu – Samweli<br>Mada – Kumsikiliza Mungu | C6 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Tatu – Samweli<br>Mada – Kumsikiliza Mungu |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***1 Samweli 3: 1-21***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Samweli 3: 10***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu alianza kusema na Samweli.<br>2. Mungu bado anazungumza na watu leo kupitia Biblia. | **Neno la Biblia:** ***1 Samweli 3: 1-21***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Samweli 3: 10***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu alianza kusema na Samweli.<br>2. Mungu bado anazungumza kupitia Biblia kwa wale wanaomsikiliza. |
| **TOA UTANGULIZI** | Waulize watoto, "Je! wana uwezo kiasi gani wa kusikiliza?" Wasomee polepole orodha ya maneno 20 kuhusu mada yoyote (k.m. chakula, wanyama, n.k.) Acha kimakusudi neno lililo dhahiri zaidi ambalo wangetarajia kusikia kuhusu mada hiyo. Ukimaliza, wape dakika 2 waandike kadiri wanavyoweza kukumbuka. Angalia ikiwa kuna mtu aliandika neno ambalo hukusema.<br>Tazama ni nani aliyepata majibu sahihi zaidi. | Waulize wanafunzi kufikiria mtu wanayemjua ambaye ni msikilizaji mzuri.<br>Kwa nini wamemchagua mtu huyo?<br>Wanawezaje kujua kuwa mtu huyo anasikiliza kweli?<br>Uliza "Je, wao ni wasikilizaji wazuri?" |
| **KAMILISHA** | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Samweli alikuwa mvulana tu ambaye bado hakuwa anamjua Mungu wakati matukio katika sura hii yalipotokea.<br>2. Usiku mmoja, alipokuwa amelala, Samweli alisikia sauti ikimwita jina lake. ***(3: 1-4)***<br>3. Akifikiri ni Eli, Samweli akainuka na kumkimbilia ili aone anachotaka. Eli alisema hakuwa amemwita. ***(3: 5-6)***<br>4. Jambo hili lilitokea mara tatu, kabla Eli hajatambua kuwa Bwana alikuwa akimwita Samweli, hivyo akamwambia Samweli nini cha kusema atakapoitwa tena. ***(3: 8-9)***<br>5. Mungu alimwita tena Samweli na wakati huu Samweli akamjibu, kama vile Eli alivyokuwa amemwambia. ***(3: 10)***<br>6. Mungu alimpa Samweli ujumbe kuhusu mambo ambayo yangeipata familia ya Eli hivi karibuni. ***(3: 11-14)***<br>7. Asubuhi Samweli alipaswa kumwambia Eli ujumbe huo. Aliogopa lakini Eli akamwambia asifiche chochote. ***(3: 15-18)***<br>8. Kwa miaka mingi, Mungu aliendelea kusema na Samweli, naye akatambuliwa kuwa nabii wa Mungu. ***(3: 19-21)***<br>9. *Elezea kuwa katika siku hizo, wakati hawana Biblia, Mungu alizungumza moja kwa moja na watu aliowachagua. Wakati mwingine waliitwa manabii na kazi yao ilikuwa ni kuleta ujumbe waliousikia na kuupeleka kwa wengine.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Tatu**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Kumsikiliza Mungu. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Samweli alikuwa mvulana tu ambaye bado hakuwa anamjua Mungu wakati matukio katika sura hii yalipotokea.<br>2. Usiku mmoja, alipokuwa amelala, Samweli alisikia sauti ikimwita jina lake. ***(3: 1-4)***<br>3. Akifikiri ni Eli, Samweli akainuka na kumkimbilia ili aone anachotaka. Eli alisema hakuwa amemwita. ***(3: 5)***<br>4. Jambo hili limetokea mara tatu, kabla Eli hajatambua kuwa Bwana alikuwa akimwita Samweli, hivyo akamwambia Samweli nini cha kusema atakapoitwa tena. ***(3: 8-9)***<br>5. Mungu alimwita tena Samweli na wakati huu Samweli akamjibu, kama vile Eli alivyokuwa amemwambia. ***(3: 10)***<br>6. Mungu alimpa Samweli ujumbe kuhusu mambo ambayo yangeipata familia ya Eli hivi karibuni. ***(3: 11-14)***<br>7. Asubuhi, Samweli alipaswa kumwambia Eli ujumbe huo. Aliogopa lakini Eli akamwambia asifiche chochote. ***(3: 15-18)***<br>8. Kwa miaka mingi, Mungu aliendelea kusema na Samweli, naye akatambuliwa kuwa nabii wa Mungu. ***(3: 19-21)***<br>9. *Eleza kuwa katika siku hizo, wakati hakuna Biblia, Mungu alizungumza moja kwa moja na watu aliowachagua. Wakati mwinginei waliitwa manabii na kazi yao ilikuwa kupeleka ujumbe waliousikia kutoka kwa Mungu na kuupeleka kwa wengine.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Tatu.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Kumsikiliza Mungu. |
| **REJELEA SOMO** | Soma ***2 Timotheo 3: 16***<br>Jadili njia ambazo Mungu anaweza kuzungumza nasi kutoka katika Biblia tunapoisoma kila siku. Ni muhimu kwa Wakristo kusoma Biblia mara kwa mara. Jadili njia za kusaidiana kufanya hivi. | Soma ***Ayubu 33: 14-18 na Luka 6: 46-49.***<br>Jadili kwa nini na jinsi gani Mungu huzungumza na watu leo. Elezea umuhimu wa Biblia. Kwa nini ni muhimu kwa Wakristo kujifunza Biblia mara kwa mara? Mkiwa wawiliwawili tafuteni njia za kusaidiana kufanya hivi. |
| **LIISHI SOMO** | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Zingatia muda unaotumia kwa sasa kuomba na kusoma Biblia - Je,unatosha? Je, unaweza kufanya zaidi?<br>2. Ikiwa huna uhakika jinsi ya kuanza kujisomea Biblia, mwombe kiongozi akusaidie. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Jiulize kama unatumia muda wa kutosha kumsikiliza Mungu na kusikia kile anachokuambia<br>2. Fanya mpango wa kuongeza muda unaotumia katika kuomba na kusoma Biblia. |

| | C6 – DARAJA LA TATU<br>Somo la Nne – Samweli<br>Mada – Kufanya Kazi ya Mungu | C6 – DARAJA LA NNE<br>Funzo la Nne – Samweli<br>Mada – Kufanya Kazi ya Mungu |
|---|---|---|
| | **Neno la Biblia:** ***1 Samweli 8: 1-9, 9: 1-8, 14-27, 10: 1***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Samweli 9: 6***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu alimwelekeza Samweli kumtia mafuta mfalme wa Israeli. Samweli alitimiza sehemu muhimu katika historia kwa sababu ya uhusiano wake na Mungu.<br>2. Maisha yetu yana kusudi tunapomfuata Mungu kwa ukaribu. | **Neno la Biblia:** ***1 Samweli 8: 1-10, 9: 1-27, 10: 1***<br><br>**Mstari Muhimu:** ***1 Samweli 9: 6***<br><br>**Tunajifunza kuwa:**<br>1. Mungu alimwelekeza Samweli kumtia mafuta mfalme wa Israeli<br>2. Mungu huongoza matukio kwa makusudi yake. Maisha yetu yanaweza kuwa na kusudi kubwa ikiwa tutamfuata Mungu kwa ukaribu. |
| TOA UTANGULIZI | Cheza mchezo mfupi wa ‘Fuata kiongozi’. Chagua mtoto awe ‘kiongozi’. Kisha awaongoze wengine kuzunguka chumba, wakifanya vitendo na kupiga kelele ambazo wengine lazima wazifuate. Cheza raundi mbili za haraka za mchezo huu, ukitumia 'kiongozi' tofauti kila wakati.<br>Warudishe watoto kwenye viti vyao na uwaombe watoe orodha ya sifa ambazo wanafikiri kiongozi mzuri anafaa kuwa nazo. Zipe namba kwa kufuata umuhimu na jadili mawazo yako na kikundi kizima. Vinginevyo, hii inaweza kufanywa na wawiliwawili. | Mkiwa wawiliwawili, orodhesheni sifa 5 ambazo kiongozi mzuri anapaswa kuwa nazo, na kisha sifa 5 za kiongozi mbaya.<br><br>Linganisha majibu pamoja na kikundi na mjadili. |
| KAMILISHA | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Inasikitisha kuwa wana wa Samweli hawakuwa tofauti na wana wa Eli, na hawakuwa viongozi wazuri wa kuchukua nafasi kutoka kwa Samweli alipokuwa mzee. ***(8: 1-3)***<br>2. Watu wa Israeli walimwomba Samweli ateue mfalme wa kuwatawala, lakini Samweli hakufurahia. ***(8: 6)***<br>3. Pia, Mungu alichukizwa kwa sababu watu walikuwa wamemkataa kama mfalme wao pekee. ***(8: 6-9)***<br>4. Mungu alimwambia Samweli awaonye watu kwa kile ambacho mfalme angefanya mara tu atakapopata mamlaka. ***(8: 10-18)*** Lakini watu walikataa kusikiliza.<br>5. Sauli, Mbenyamini, akatoka kwenda kuwatafuta punda wa baba yake waliopotea. Alisafiri maili nyingi lakini hakuwapata. ***(9: 1-5)***<br>6. Mtumishi wa Sauli alipendekeza kuwa waende kwa Samweli ili kupata msaada kwa sababu alikuwa nabii wa Mungu aliyeheshimiwa. ***(9: 6)***<br>7. Mungu alimwongoza Sauli kukutana na Samweli na kumwambia Samweli kuwa huyo ndiye mtu aliyemchagua kuwa mfalme. Samweli alikula pamoja na Sauli kisha akampaka mafuta awe mfalme. ***(9: 14-27, 10: 1)***<br>8. *Samweli alikuwa nabii na mwamuzi mkuu. Siri ya ukuu wake ilikuwa uhusiano wake wa karibu na Mungu. Maisha yetu pia yanaweza kuwa na manufaa tunapomruhusu Mungu ayatawale kikamilifu.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Somo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Kufanya kazi ya Mungu. | **Wasilisha Habari ya Biblia**<br><br>**Jadili na Uelezee:**<br>1. Inasikitisha kuwa wana wa Samweli hawakuwa tofauti na wana wa Eli, na hawakuwa viongozi wazuri wa kuchukua nafasi kutoka kwa Samweli alipokuwa mzee. ***(8: 1-3)***<br>2. Watu wa Israeli walimwomba Samweli ateue mfalme wa kuwatawala, lakini Samweli hakufurahia. ***(8: 6)***<br>3. Pia, Mungu alichukizwa kwa sababu watu walikuwa wamemkataa kama mfalme wao pekee. ***(8: 6-9)***<br>4. Alimwambia Samweli awaonye watu kwa kile ambacho mfalme angefanya mara tu atakapopata mamlaka. ***(8: 10-18)***. Lakini watu walikataa kusikiliza.<br>5. Sauli, Mbenyamini, akatoka kwenda kuwatafuta punda wa baba yake waliopotea. Alisafiri maili nyingi lakini hakuwapata. ***(9: 1-5)***<br>6. Mtumishi wa Sauli alipendekeza kuwa waende kwa Samweli ili kupata msaada kwa sababu alikuwa nabii wa Mungu aliyeheshimiwa. ***(9: 6)***<br>7. Mungu alimwongoza Sauli kukutana na Samweli na kumwambia Samweli kwamba huyo ndiye mtu aliyemchagua kuwa mfalme. Samweli alikula pamoja na Sauli kisha akampaka mafuta awe mfalme. ***(9: 14-27, 10: 1)***<br>8. *Samweli alikuwa nabii na mwamuzi mkuu. Siri ya ukuu wake ilikuwa uhusiano wake wa karibu na Mungu. Maisha yetu pia yanaweza kuwa na manufaa tunapomruhusu Mungu ayatawale kikamilifu.*<br><br>**Elezea Mstari Muhimu na wahamasishe wanafunzi kujifunza.**<br>**Kamilisha Funzo la Nne.**<br>**Onesha:** Angalia linki/ kiungo cha FBI kwenye kiambatisho C – Kufanya kazi ya Mungu. |
| REJELEA SOMO | Jadili: Umejifunza nini kutokana na somo hili kuhusu jinsi ya kukuza uhusiano wako na Mungu?<br>Fikiria juu ya sifa ambazo Samweli alikuwa nazo unazozipenda. Tengeneza bango ili kuzionyesha, kwa kutumia maneno au picha, au mchanganyiko wa vyote viwili. | Soma ***Zaburi 15***. Mungu anataka tuwe watu wa aina gani? Tengeneza meza yenye safu mbili. Katika safu moja, orodhesha mambo yote ambayo Zaburi hii inasema kwamba tufanye; katika safu ya pili, orodhesha mambo ambayo Zaburi inasema tusiyafanye. |
| LIISHI SOMO | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>Mwombe Mungu akusaidie kukuza uhusiano wako naye na kutimiza makusudi yake maishani mwako, kama alivyofanya na Samweli. | **Kwa namna gani somo hili linatupa changamoto?**<br>1. Mshukuru Mungu kuwa anaweza kuelekeza matukio katika maisha yetu kwa makusudi yake, kama alivyofanya na Samweli.<br>2. Mwombe Mungu akusaidie kuwa mtu ambaye anataka uwe ili kutimiza makusudi yake maishani mwako. |

## Maelezo ya Walimu Wanaposaisha Masomo

**Masomo ya Daraja la Tatu**

- Wanafunzi hawawezi kumaliza masomo haya bila kurejelea Biblia na huenda wakalazimika kurejea moja au zaidi ya Usomaji wa Biblia.
- Kuna maswali ya aina mbalimbali pamoja na maneno ya msalaba na gridi za maneno, maneno yanayokosekana, n.k.
- Yameundwa hasa kujibiwa kwa Biblia za matoleo ya NIV, Habari Njema, RSV New King James, Authorized Version na matoleo ya kawaida ya Bibilia ya Kiingereza.
- Lengo letu ni kwamba wanafunzi wote, kwa kutumia Biblia yoyote waliyo nayo, waweze kujibu maswali.
- Alama ishirini zimetengwa kwa kila wiki ambapo kiwango cha juu ni 80 kwa mwezi, pale masomo yanapofanyika kwa usahihi kabisa.
- Daraja la Tatu - Kwa kawaida alama 1 kwa kila jibu inahitajika, kama ilivyoelekezwa.

**Mafunzo ya Daraja la Nne**

- Hili ni toleo gumu zaidi baada ya masomo ya Daraja la Tatu.
- Maswali magumu zaidi na majibu ya kina zaidi yanahitajika.
- Alama ishirini kwa wiki na 80 kwa mwezi, pale masomo yanapofanyika kwa usahihi kabisa, na maswali yanapojibiwa kwa ukamilifu.

**VIDOKEZO VYA USAISHAJI**

Walimu wanatakiwa, kwanza:

- Kupitia kila somo na kutambua majibu sahihi au yasiyo sahihi.
- Kutuza pointi muhimu kama ilivyoelekezwa.
- Kusaisha kila wakati kwa rangi tofauti na KUWEKA TIKI katika kila jibu sahihi.
- Kuingiza jibu sahihi, inapofaa na kurekebisha makosa yoyote ya tahajia, ingawa HAKUNA alama zinazopunguzwa kwa marekebisho haya.
- Kupatia alama chache kwa majibu ambayo usahihi wake sio kamili.
- Kujumlisha alama zote za mwezi na kuandika jumla hiyo kwenye ukurasa wa nyuma katika nafasi iliyotolewa.

Inahitajika kuwa mkarimu na kufanya kila linalowezekana kuwatia moyo wanafunzi waendelee na Mafunzo yao ya Biblia.

Inasaidia, pale inapowezekana kila mwezi kwa mwalimu kuandika neno la kumtia moyo mwanafunzi na kuna nafasi iliyotolewa kwenye karatasi ya somo kwa ajili ya hili kufanyika. Maoni yanaweza kutolewa kuhusu upakaji wa rangi nzuri, unadhifu, alama zilizopatikana, uelewa wa mwanafunzi wa somo, nk.

Tunajaribu kutoa maoni tofauti kadri iwezekanavyo. Maswali, maelezo, ugunduzi, kutia moyo, n.k vyote vinaweza kutumiwa kuleta utofauti. Tunahitaji ubunifu, lakini ni muhimu kuweka mbele masilahi ya mwanafunzi. Ikiwa tunarudia maelezo au swali hilohilo kila mwezi, linapoteza mguso wake kwa wanafunzi.

**DARAJA LA TATU**

**Maoni ya jumla**

“Kazi njema! Ni wazi kwamba ulisoma maswali kwa uangalifu sana. Nimependa sana jibu lako kwa swali la mwisho ambalo lilikuwa na maneno mazuri sana.”

“Halo Yonathani. Asante kwa bidii yako yote. Umefanya vizuri kuweza kupata takriban majibu yote. Nimekujazia majibu ambayo ulishindwa kujibu."

**Maoni ya kiroho**

"Musa alikuwa na wakati mgumu na wana wa Israeli, lakini Mungu hakumwacha atatue shida zote peke yake."

“Yusufu hakusahau kuwa baba yake alikuwa amemfundisha kumpenda Mungu. Alikumbuka hili hata wakati akiwa mbali na nyumbani.”

“Bartimayo alikuwa amedhamiria kufika kwa Bwana Yesu. "Hakukata tamaa kwa kuwa sasa alikuwa anaweza kuona na wakati huu alijua Bwana Yesu alikuwa mtu wa kipekee sana."

**DARAJA LA NNE**

**Maoni ya jumla**

“Seti nyingine ya masomo yaliyojibiwa kwa ubora. Unaonekana kuwa na ufahamu mzuri juu ya habari hizi za Biblia na natumaini kuwa umezifurahia. Asante kwa kutumia muda wako kufanya masomo kwa uangalifu. Ungeweza kuamua kuyapitia juujuu kwa haraka, kwa hiyo natambua bidii yako yote. ”

“Umejaribu vizuri sana, Raheli. Nadhani kwa majibu yako, labda haujaelewa vizuri habari hiyo. Pengine ungejaribu kuisoma tena.”

**Maoni ya kiroho**

"Mifano ya Biblia wakati mwingine huitwa habari za kidunia zenye maana ya mbinguni, au ya kina. Je! Unaweza kufikiria mfano kwenye funzo la tatu una maana gani ya kina? ”

"Stefano alikufa kifo cha kikatili na bado hakuogopa kufa, kwa vile alijua kwamba Mungu yupo na alijua atakuwa na Bwana Yesu Mbinguni."

| Kiambatisho A – Daraja la Tatu Picha kutoka Free Bible Images | | |
|---|---|---|
| | Kichwa cha Habari | Picha za Habari |
| C1 | Danieli | **Nchi ya ugenini** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/daniel-food/ |
| | | **Tanuru ya moto** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/meshach-shadrach-abednego/ |
| | | **Mkono wa ajabu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/daniel-feast/ |
| | | **Tundu la simba** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/daniel-lions/ |
| | | |
| C2 | Watu aliokutana nao Yesu | **Yesu akutana na mtu huko Yeriko** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/lgr-zacchaeus/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-077-zacchaeus/ |
| | | **Yesu akutana na mwanamke kisimani** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-samaritan-woman/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-018-samaritan-woman/ |
| | | **Yesu akutana na mtu usiku** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-017-nicodemus/ |
| | | **Yesu akutana na kipofu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-blind-man/ |

| Kiambatisho A – Daraja la Nne kutoka Free Bible Images | | |
|---|---|---|
| | Kichwa cha habari | Picha za Habari |
| C1 | Danieli | **Kumtumikia Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/daniel-food/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/daniel-dream/ |
| | | **Kusimama imara katika Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/meshach-shadrach-abednego/ |
| | | **Kusema kwa ajili ya Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/daniel-feast/ |
| | | **Kuteseka kwa ajili ya Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/daniel-lions/ |
| | | |
| C2 | Maneno ya Yesu | **Kuhusu dhambi** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/zacchaeus/ |
| | | **Kuhusu kuona** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/blind-man/ |
| | | **Kuhusu wachungaji** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-063-good-shepherd/ |
| | | **Kuhusu Wokovu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-017-nicodemus/ |

## Kiambatisho B – Daraja la Tatu Picha kutoka Free Bible Images

| | Kichwa cha habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| C3 | Miujiza Zaidi | **Yesu amsaidia mgonjwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-jesus-bethesda/ |
| | | **Yesu amsaidia mtu mwenye huzuni** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jairus-daughter/ |
| | | **Yesu amsaidia mtumishi wa akida** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-jesus-centurion/ |
| | | **Yesu asaidia umati wenye njaa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-feeding-5000/ |
| | | |
| C4 | Kifo cha Kristo | **Busu la Msaliti** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-089-prayer-garden/ |
| | | **Maamuzi ya Liwali** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-093-mocking-jesus/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-094-pilate/ |
| | | **Kaburi la Tajiri** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-099-jesus-burial/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-101-jesus-resurrection/ |
| | | **Maneno ya Mgeni** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-103-appearance-emmaus/ |

## Kiambatisho B – Daraja la Nne kutoka Free Bible Images

| | Kichwa cha habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| C3 | Nguvu za Bwana | **Kuponya mgonjwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-bethesda/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-029-lame-man/ |
| | | **Kufufua wafu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-045-two-miracles/ |
| | | **Kusaidia wahitaji** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-centurion/ |
| | | **Kulisha wenye njaa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/feeding-5000/ |
| | | |
| C4 | Kifo cha Kristo | **Ahukumiwa na Kusulubiwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-trials/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-crucified-dies/ |
| | | **Azikwa na Kufufuka!** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/gnpi-099-jesus-burial/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/jesus-resurrection/ |
| | | **Aonekana na Kusikika** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/disciples-emmaus/ |
| | | **Atiliwa Mashaka na Kuaminiwa** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/resurrection-appearances/ |

## Kiambatisho C – Daraja la Tatu Picha kutoka Free Bible Images

| | Kichwa cha habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| C5 | Ruthu | **Maamuzi Mabaya** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ruth-1/ |
| | | **Kurudi kwa Wajane** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ruth-1/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ruth-2/ |
| | | **Familia Tajiri** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ruth-2/ |
| | | **Mapenzi ya Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ruth-3/ |
| | | |
| C6 | Samweli | **Kumwomba Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/yo-samuel-saul/ |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/samuel-born/ |
| | | **Kukua mbele za Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/samuel-listens/ |
| | | **Kumsikiliza Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/samuel-listens/ |
| | | **Kufanya kazi ya Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/samuel-saul/ |

## Kiambatisho C – Daraja la Nne kutoka Free Bible Images

| | Kichwa cha habari | Picha za Habari |
|---|---|---|
| C5 | Ruthu | **Familia kuwa mbali na Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ruth-1/ |
| | | **Naomi amrudia Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ruth-1/ |
| | | **Wajane waongozwa na Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ruth-2/ |
| | | **Boazi na Ruthu wabarikiwa na Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/ruth-3/ |
| | | |
| C6 | Samweli | **Kumwomba Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/samuel-born/ |
| | | **Kukua mbele za Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/samuel-listens/ |
| | | **Kumsikiliza Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/samuel-listens/ |
| | | **Kufanya kazi ya Mungu** |
| | | https://www.freebibleimages.org/illustrations/samuel-saul/ |

© Bible Educational Services 2020

www.besweb.com

Registered Charity UK CIO 1186004

Swahili - 12/2023